# MAELEKEZO KWA WASIMAMIZI WA UCHAGUZI

# YALIYOMO

**UJUMBE WA MWENYEKITI** ........ viii

**DIBAJI** ........ ix

**SURA YA KWANZA** ........ 1

**UTEUZI WA WATENDAJI WA UCHAGUZI** ........ 1

1.1. Uteuzi wa Waratibu wa Uchaguzi wa Mikoa ........ 1

1.2. Uteuzi wa Wasimamizi wa Uchaguzi ........ 1

1.3. Uteuzi wa Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi ........ 1

1.4. Maafisa Uchaguzi ........ 1

1.5. Uwajibikaji wa Watendaji ........ 2

1.6. Kiapo na Tamko ........ 2

**SURA YA PILI** ........ 3

**MAJUKUMU YA WARATIBU WA UCHAGUZI WA MIKOA NA WASIMAMIZI WA UCHAGUZI** ........ 3

2.1. Waratibu wa Uchaguzi wa Mikoa ........ 3

2.2. Msimamizi wa Uchaguzi ........ 3

**SURA YA TATU** ........ 6

**DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA** ........ 6

3.1. Daftari na Orodha ya Wapiga Kura ........ 6

3.2. Mpiga Kura Kutambua Kituo chake cha Kupigia Kura ........ 6

**SURA YA NNE** ........ 8

**UTEUZI WA WAGOMBEA WA KITI CHA RAIS NA MAKAMU WA RAIS** ........ 8

4.1. Siku ya Uteuzi ........ 8

4.2. Sifa za Mgombea wa Kiti cha Rais na Makamu wa Rais ........ 8

4.3. Masharti ya Uteuzi wa Wagombea wa Kiti cha Rais na Makamu wa Rais ........ 8

4.4 Masharti ya Urejeshaji wa Dhamana za Wagombea ........ 9

4.5. Fomu za Uteuzi (Fomu Na. 8A) ........ 9

4.6. Wadhamini wa Wagombea ........ 10

4.7. Msimamizi wa Uchaguzi Kuthibitisha Wadhamini wa Mgombea ..................10
4.8. Uwasilishaji wa Fomu Siku ya Uteuzi ..................10
4.9. Pingamizi Dhidi ya Uteuzi wa Mgombea wa Kiti cha Rais na Makamu wa Rais ..................11
4.10. Uamuzi wa Tume ..................13
4.11. Kutokuwepo au Kufariki kwa Mgombea ..................13
4.12 . Mgombea Pekee wa Kiti cha Rais ..................14
4.13. Kujitoa kwa Mgombea ..................14

**SURA YA TANO ..................15**

**UTEUZI WA WAGOMBEA UBUNGE ..................15**

5.1. Siku ya Uteuzi ..................15
5.2. Sifa za Mgombea Ubunge ..................15
5.3. Kukosa Sifa za Kugombea Ubunge ..................16
5.4. Masharti ya Uteuzi wa Mgombea Ubunge ..................17
5.5. Dhamana za Wagombea ..................17
5.6. Fomu ya Uteuzi (Fomu Na. 8B) ..................18
5.7. Utoaji wa Fomu za Uteuzi ..................18
5.8. Uwasilishaji wa Fomu Siku ya Uteuzi ..................18
5.9. Utaratibu wa Kushughulikia Fomu za Uteuzi ..................19
5.10. Mpiga Kura Aliyedhamini Zaidi ya Mgombea Mmoja ..................20
5.11. Pingamizi Dhidi ya Uteuzi wa Mgombea Ubunge ..................21
5.12. Utaratibu wa Kushughulikia Pingamizi ..................23
5.13. Utaratibu wa Msimamizi wa Uchaguzi Kuweka Pingamizi Dhidi ya Uteuzi wa Mgombea ..................23
5.14. Utaratibu wa Kukata Rufaa ..................24
5.15. Kuwasilisha Fomu za Uteuzi Tume ..................24
5.16. Kutokuwepo kwa Wagombea ..................25
5.17. Mgombea Aliyepita Bila Kupingwa ..................25
5.18. Kujitoa kwa Mgombea ..................25
5.19. Kufariki kwa Mgombea ..................25

**SURA YA SITA** ........................................................................................ **26**

**UTEUZI WA WAGOMBEA UDIWANI** ........................................................ **26**

6.1. Siku ya Uteuzi ........................................................................................ 26

6.2. Sifa za Mgombea Udiwani ........................................................................ 26

6.3. Kukosa Sifa za Kugombea Udiwani .......................................................... 26

6.4. Masharti ya Uteuzi wa Mgombea Udiwani ................................................ 27

6.5. Fomu ya Uteuzi ( Fomu Na. 8C) ............................................................... 28

6.6. Utoaji wa Fomu za Uteuzi ........................................................................ 28

6.7. Uwasilishaji wa Fomu Siku ya Uteuzi. ...................................................... 28

6.8. Utaratibu wa Kushughulikia Fomu za Uteuzi ............................................ 29

6.9. Mpiga Kura Anayedhamini Mgombea Udiwani Zaidi ya Mmoja ................. 30

6.10. Pingamizi Dhidi ya Uteuzi wa Mgombea Udiwani .................................... 31

6.11. Utaratibu wa Kuwasilisha Rufaa. ............................................................. 34

6.12. Kuwasilisha Fomu za Uteuzi Tume .......................................................... 34

6.13. Kutokuwepo kwa Wagombea ................................................................... 35

6.14. Mgombea Aliyepita bila Kupingwa ........................................................... 35

6.15. Kujitoa kwa Mgombea ............................................................................. 35

**SURA YA SABA** ..................................................................................... **36**

**UTARATIBU WA WATUMISHI WA UMMA KUGOMBEA UBUNGE NA UDIWANI** ........................................................................................ **36**

7.1. Wanaoruhusiwa na Wasioruhusiwa Kugombea Miongoni mwa Watumishi wa Umma ........................................................................................ 36

7.2. Wakati wa Kujitayarisha Kugombea ......................................................... 37

7.3. Baada ya Kuteuliwa au Kutangazwa na Tume ......................................... 37

**SURA YA NANE** ..................................................................................... **38**

**KAMPENI ZA UCHAGUZI** ...................................................................... **38**

8.1 Kipindi cha Kampeni .................................................................................. 38

8.2. Wajibu wa Tume Katika Kuratibu Ratiba ya Kampeni za Wagombea wa Kiti cha Rais na Makamu wa Rais .......................................................... 38

8.3. Wajibu wa Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi katika Kuratibu Ratiba za Kampeni za Wagombea Ubunge na Udiwani .........39
8.4. Wajibu wa Mgombea, Chama cha Siasa na Wakala Wakati wa Kampeni ........40
8.5. Maelekezo ya Jumla Kuhusu Kampeni ........41
8.6. Maadili ya Uchaguzi ........41
**SURA YA TISA ........43**
**UPIGAJI KURA ........43**
9.1 Maandalizi Kuelekea Siku ya Upigaji Kura ........43
9.2. Vituo vya Kupigia Kura ........43
9.3. Tangazo la Uchaguzi (*Notice of Election*) ........44
9.4. Uteuzi wa Watendaji wa Vituo vya Kupigia Kura ........45
9.5. Utaratibu wa Kuteua Watendaji wa Kituo ........46
9.6. Walinzi wa Vituo ........46
9.7. Mafunzo kwa Wasimamizi wa Vituo na Wasimamizi Wasaidizi wa Vituo na Makarani Waongozaji Wapiga Kura ........46
9.8. Uteuzi na Wajibu wa Mawakala wa Upigaji Kura ........47
9.9. Fomu na Vifaa vya Upigaji Kura ........49
9.10. Makabidhiano na Usalama wa Vifaa vya Kupigia Kura ........54
9.11. Vibali vya Watendaji wa Uchaguzi, Mawakala na Wagombea Kupiga Kura Vituo Ambavyo Hawakujiandikisha Fomu Na. 18 na Na. 19 ........55
9.12. Kuahirisha Upigaji Kura ........56
9.13. Siku ya Kupiga Kura ........56
9.14. Namna ya Kuendesha Zoezi la Upigaji Kura ........56
9.15. Matumizi ya Fomu Na. 17 ........57
9.16. Wanaoruhusiwa Kuingia Kwenye Kituo cha Kupigia Kura ........58
9.17. Utaratibu wa Kufunga Kituo ........58
9.18. Kuhesabu Kura ........59
9.18.1 Alama Zinazokubalika Katika Karatasi ya Kura ........60
9.18.2 Uamuzi wa Kuwa Kura ni Halali au Siyo Halali ........60
9.18.3 Kura Zilizoharibika ........61
9.19. Ujazaji wa Fomu ya Matokeo ya Uchaguzi Kituoni ........61

**SURA YA KUMI ........................................................................................65**
**KUJUMLISHA KURA........................................................................................ 65**
10.1. Wanaoruhusiwa Kuwepo Wakati wa Kujumlisha Kura ....................................65
10.2. Maandalizi katika Sehemu ya Kujumlisha Kura..................................................65
10.3. Utaratibu wa Kufuata Kabla ya Kuanza Kujumlisha Kura ................................68
10.4. Utaratibu wa Kufuata Wakati wa Kujumlisha Kura ...........................................68
10.5. Kutoa Uamuzi Kuhusu Kura zenye Mgogoro......................................................69
10.6. Maombi ya Wakala au Mgombea ya Kurudia Kuhesabu Kura..........................69
10.7. Kulingana kwa Kura za Wagombea .......................................................................69
10.8. Kujumlisha Kura za Madiwani...............................................................................70
10.9. Mawakala wa Kujumlisha Kura .............................................................................70
**SURA YA KUMI NA MOJA..........................................................................71**
**KUTANGAZA MATOKEO YA UCHAGUZI ................................................... 71**
11.1. Taarifa ya Msimamizi wa Uchaguzi .......................................................................71
11.2. Kuhifadhi Nyaraka za Uchaguzi Zilizotumika ....................................................72
**SURA YA KUMI NA MBILI..........................................................................73**
**MAKOSA YA UCHAGUZI............................................................................... 73**
**SURA YA KUMI NA TATU ...........................................................................75**
**ELIMU YA MPIGA KURA............................................................................... 75**
13.1. Utaratibu wa Kutoa Elimu kwa Mpiga Kura.........................................................75
**SURA YA KUMI NA NNE..............................................................................77**
**HITIMISHO ....................................................................................................... 77**

# UJUMBE WA MWENYEKITI

Umeteuliwa kuwa Msimamizi wa Uchaguzi, nafasi ambayo ina majukumu mazito yenye heshima na dhamana kubwa kitaifa katika uendeshaji wa uchaguzi. Ili kufanikisha utekelezaji wa majukumu hayo, Tume ya Taifa ya Uchaguzi imeteua watendaji wengine ambao watakusaidia kutekeleza shughuli za uchaguzi katika halmashauri yako kwa ngazi ya jimbo na kata.

Katika utekelezaji wa majukumu yako ya kiuchaguzi unapaswa uzingatie Katiba ya Nchi, Sheria za Uchaguzi na Kanuni zake, Maadili ya Uchaguzi na Maelekezo mbalimbali yanayotolewa na Tume. Aidha, ili kufanikisha majukumu hayo ni muhimu kuvishirikisha vyama vya siasa na wadau wengine wa uchaguzi katika masuala ambayo wanastahili kushirikishwa.

Ukizingatia hayo, utawezesha kuwa na uchaguzi huru, wa haki, wa wazi na wa kuaminika. Hivyo, utakuwa umechangia katika kuilinda amani na kukuza demokrasia nchini.

Nakutakia kila la kheri na mafanikio katika kazi hii.

JAJI WA RUFAA (MST.) SEMISTOCLES S. KAIJAGE
*Mwenyekiti*
*Tume ya Taifa ya Uchaguzi*

# DIBAJI

Kwa mujibu wa kifungu cha 126 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, Tume imepewa mamlaka ya kuandaa maelekezo mbalimbali kwa ajili ya watendaji wa uchaguzi ili kuwezesha utekelezaji bora wa majukumu yao.

Hivyo, maelekezo haya yameandaliwa kuwawezesha Waratibu wa Uchaguzi wa Mikoa, Wasimamizi wa Uchaguzi na Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi kusimamia uendeshaji wa uchaguzi kwenye maeneo yao.

Maelekezo yaliyomo katika kitabu hiki yamebainisha namna ya kutekeleza kwa ufanisi shughuli za msingi zinazofanyika katika kipindi cha uchaguzi ambazo ni pamoja na uteuzi wa wagombea, uteuzi wa watendaji wa vituo, kampeni za uchaguzi, usimamizi wa Maadili ya Uchaguzi, ugawaji na usambazaji wa vifaa vya uchaguzi, zoezi la upigaji kura, kuhesabu kura, kujumlisha kura na kutangaza matokeo ya uchaguzi.

Hivyo, pamoja na maelekezo haya, Waratibu wa Uchaguzi wa Mikoa, Wasimamizi wa Uchaguzi na Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi ngazi ya jimbo na kata mnapaswa pia kuzingatia:-

(i) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977;

(ii) Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343;

(iii) Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292;

(iv) Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287;

(v) Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288;

(vi) Sheria ya Gharama za Uchaguzi, Sura ya 278;

(vii) Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2020;

(viii) Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020;

(ix) Vijitabu vingine vya maelekezo vilivyotolewa na Tume, yaani: -

- Maelekezo kwa Wasimamizi wa Vituo vya Kupigia Kura;
- Maelekezo kwa Vyama vya Siasa na Wagombea;
- Maelekezo kwa Makarani Waongozaji Wapiga Kura;
- Maelekezo kwa Mawakala wa Vyama vya Siasa;
- Mwongozo wa utoaji wa Elimu ya Mpiga Kura;

- Maadili ya Uchaguzi ya mwaka 2020;
- Mwongozo wa Watazamaji wa Uchaguzi; na
- Maelekezo mengine yatakayotolewa na Tume.

Tume inatarajia kuwa mtatekeleza majukumu mliyopewa kwa ufanisi na weledi. Aidha, Tume itakuwa tayari kutoa ufafanuzi wa suala lolote pale itakapohitajika.

DKT. WILSON MAHERA CHARLES
*Mkurugenzi wa Uchaguzi*

# SURA YA KWANZA

## UTEUZI WA WATENDAJI WA UCHAGUZI

### 1.1. Uteuzi wa Waratibu wa Uchaguzi wa Mikoa

Kwa mujibu wa kifungu cha 8(1) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, Tume inaweza kuteua Waratibu wa Uchaguzi wa Mikoa kwa nyadhifa zao au kwa majina yao kwa ajili ya kuratibu shughuli za uchaguzi katika mikoa.

### 1.2. Uteuzi wa Wasimamizi wa Uchaguzi

Kwa lengo la kusimamia uchaguzi na kwa kuzingatia kifungu cha 7(1) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, na kifungu cha 9(1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, Wakurugenzi wa Halmashauri za Majiji; Wakurugenzi wa Halmashauri za Manispaa; Wakurugenzi wa Halmashauri za Miji; na Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri za Wilaya watakuwa Wasimamizi wa Uchaguzi kwa nyadhifa zao.

Kwa mujibu wa kifungu cha 7(3) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, na kifungu cha 9(6) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, Tume inaweza kumteua mtumishi mwingine yeyote wa umma kwa jina au kwa wadhifa kuwa Msimamizi wa Uchaguzi pale inaporidhika kwamba kwa mazingira yaliyopo Mkurugenzi aliyetajwa katika sheria hawezi kusimamia uchaguzi. Iwapo Tume itaamua kufanya hivyo, Mkurugenzi wa Halmashauri husika hatakuwa Msimamizi wa Uchaguzi.

### 1.3. Uteuzi wa Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi

Kwa mujibu wa kifungu cha 7(2) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, na kifungu cha 9(2) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, Tume inaweza kuwateua kwa nyadhifa au kwa majina Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi ngazi ya jimbo na kata miongoni mwa watumishi wa umma kwa idadi itakayoona inafaa. Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi watatekeleza majukumu yao chini ya Wasimamizi wa Uchaguzi. Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi anaweza kutekeleza majukumu ya Msimamizi wa Uchaguzi.

### 1.4. Maafisa Uchaguzi

Kwa kuzingatia kifungu cha 8(2) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, Tume huwatumia Maafisa Uchaguzi waliopo katika halmashauri

kuwasaidia Wasimamizi wa Uchaguzi. Maafisa Uchaguzi watatekeleza majukumu ya kiutawala yanayohusiana na uchaguzi kwa kufuata maelekezo ya Msimamizi wa Uchaguzi.

### 1.5. Uwajibikaji wa Watendaji

Waratibu wa Uchaguzi wa Mikoa na Wasimamizi wa Uchaguzi wanawajibika kwa Tume. Aidha, Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi ngazi ya jimbo na kata na Maafisa Uchaguzi wanawajibika kwa Msimamizi wa Uchaguzi.

### 1.6. Kiapo na Tamko

Kabla ya kuanza kutekeleza majukumu yao, Waratibu wa Uchaguzi wa Mikoa, Wasimamizi wa Uchaguzi, Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi ngazi ya jimbo na kata na Maafisa Uchaguzi wanatakiwa kuapa kiapo cha kutunza siri na kutoa tamko la kujitoa uanachama au kutokuwa mwanachama wa chama cha siasa mbele ya Hakimu kama ifuatavyo: -

**(i) Kiapo cha Kutunza Siri**

Kiapo cha kutunza siri hutolewa kwa mujibu wa kifungu cha 7(5) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 9(5) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292. Aidha, kwa mujibu wa kanuni ya 16(1) (a) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2020 na kanuni ya 14 (1) (a) ya Kanuni za Uchaguzi ya Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020 kiapo hicho hutolewa katika Fomu Na. 6.

**(ii) Tamko la Kujitoa Uanachama au Kutokuwa Mwanachama wa Chama cha Siasa**

Tamko hili hutolewa kwa mujibu wa kanuni ya 16(1)(b) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2020 na kanuni ya 14 (1)(b) ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020 kwa kujaza Fomu Na. 7.

# SURA YA PILI

## MAJUKUMU YA WARATIBU WA UCHAGUZI WA MIKOA NA WASIMAMIZI WA UCHAGUZI

### 2.1. Waratibu wa Uchaguzi wa Mikoa

Kwa mujibu wa kifungu cha 8 (1) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, kikisomwa pamoja na kanuni ya 9(1) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2020 na kanuni ya 7(1) ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020 majukumu ya Mratibu wa Uchaguzi wa Mkoa ni:-

(i) Kuratibu taarifa mbalimbali zinazohusiana na uchaguzi katika halmashauri au majimbo yaliyopo katika mkoa;

(ii) Kuratibu na kuhakikisha vifaa vya uchaguzi vinapatikana kwa idadi inayohitajika na kwa muda uliopangwa; na

(iii) Kuratibu upatikanaji wa rasilimali na mambo mengine muhimu yanayohitajika kwa ajili ya kufanikisha uchaguzi katika halmashauri au majimbo yote kwenye mkoa.

Aidha, katika kutekeleza majukumu yake Mratibu wa Uchaguzi wa Mkoa atatakiwa kushirikiana na kushauriana na Wasimamizi wa Uchaguzi waliopo katika mkoa.

### 2.2. Msimamizi wa Uchaguzi

Majukumu ya Msimamizi wa Uchaguzi ni pamoja na:-

(i) Kuwa kiongozi mkuu kiutawala na kisheria katika shughuli zote za uchaguzi ndani ya halmashauri, majimbo na kata;

(ii) Kupokea vifaa kutoka Tume, kuvihifadhi na kusambaza kwenda katika vituo vya kupigia kura, pia kukusanya na kuhifadhi vifaa hivyo katika hali ya usalama baada ya uchaguzi;

(iii) Kusimamia fedha za uchaguzi na kufanya matumizi yote ya fedha hizo kwa mujibu wa Sheria za Fedha za Umma, Sheria ya Manunuzi ya Umma, Sheria za Uchaguzi na Maelekezo ya Tume;

(iv) Kuteua na kuwaapisha watendaji wa vituo watakaomsaidia katika utekelezaji wa shughuli za uchaguzi kwa idadi itakayoelekezwa na Tume. Watendaji hao ni: -

(a) Wasimamizi wa Vituo vya Kupigia Kura (*Presiding Officers*);

(b) Wasimamizi Wasaidizi wa Vituo vya Kupigia Kura (*Polling Assistants*);

(c) Walinzi wa Vituo vya Kupigia Kura; na

(d) Makarani Waongozaji Wapiga Kura (*Direction Clerks*).

(v) Kuwaapisha mawakala wa vyama vya siasa na kuwatambulisha kwa watendaji wa vituo vya kupigia kura;

(vi) Kuratibu na kusimamia utoaji wa Elimu ya Mpiga Kura katika majimbo na kata zilizopo katika halmashauri yake kwa mujibu wa maelekezo ya Tume;

(vii) Kutoa mafunzo kwa Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata, Wasimamizi wa Vituo vya Kupigia Kura, Wasimamizi Wasaidizi wa Vituo vya Kupigia Kura na Makarani Waongozaji Wapiga Kura;

(viii) Kutoa fomu za uteuzi kwa wagombea waliopendekezwa na vyama vyao;

(ix) Kuteua wagombea Ubunge na Udiwani;

(x) Kushughulikia pingamizi za wagombea;

(xi) Kutoa fomu za rufaa na kuzipokea kwa niaba ya Tume;

(xii) Kuratibu kampeni za wagombea ngazi ya jimbo na kata;

(xiii) Kusimamia utekelezaji wa Maadili ya Uchaguzi katika jimbo na kata;

(xiv) Kutoa Tangazo la Uchaguzi (*Notice of Election*) katika halmashauri, jimbo, kata na kituo;

(xv) Kuhakikisha kuwa anafanikisha uchaguzi katika halmashauri, jimbo na kata kwa kuandaa mipango mizuri ya uendeshaji wa uchaguzi. Ili aweze kufanya hivyo kwa ufanisi, ni muhimu ayaelewe vema mazingira ya jimbo na kata yanayoweza kuathiri uchaguzi katika hatua mbalimbali. Mambo anayotakiwa kuyaelewa na kuyatafakari kwa umakini ni pamoja na:-

(a) Hali ya kijiografia;

(b) Hali ya usafiri na mawasiliano;

(c) Hali ya kisiasa na kijamii;

(d) Hali ya kiuchumi; na

(e) Matukio mbalimbali yaliyowahi kutokea na yanayoweza kuathiri ufanisi wa uchaguzi kwa ujumla.

(xvi) Kufanya maandalizi ya vituo vya kupigia kura;

(xvii) Kusimamia zoezi la kupiga kura, kuhesabu kura, kujumlisha kura, kutangaza matokeo ya uchaguzi na kutuma matokeo hayo Tume kwa haraka;

(xviii) Kushirikiana na kushauriana na Mratibu wa Uchaguzi wa Mkoa;

(xix) Kuandaa taarifa ya mwenendo wa zoezi zima la uchaguzi na kuiwasilisha Tume katika kipindi kisichozidi mwezi mmoja baada ya uchaguzi;

(xx) Kuandaa taarifa ya mapokezi na matumizi ya fedha za uchaguzi na kuiwasilisha Tume si zaidi ya miezi miwili baada ya uchaguzi; na

(xxi) Kutekeleza majukumu mengine yoyote ya kiuchaguzi kama itakavyoelekezwa na Tume au Mkurugenzi wa Uchaguzi.

**Angalizo:**

Katika kufanya uteuzi wa watendaji waliotajwa kwenye kipengele cha 2.2 (iv), Tume inashauri kutoa kipaumbele kwa makundi maalum kama vile wanawake, vijana na watu wenye ulemavu wenye uwezo wa kufanya kazi za uchaguzi.

# SURA YA TATU

## DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA

### 3.1. Daftari na Orodha ya Wapiga Kura

Tume itawapatia Wasimamizi wa Uchaguzi Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na orodha ya wapiga kura kwa kila kituo cha kupigia kura. Daftari hilo ndilo litakalotumika Siku ya Uchaguzi.

Tume itatoa nakala tete (*soft copy*) ya Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa vyama vya siasa. Hata hivyo, Daftari rasmi litakalotumika Siku ya Uchaguzi katika kila kituo ni lile litakalotolewa na Msimamizi wa Uchaguzi.

Daftari la Kudumu la Wapiga Kura litaonesha wapiga kura wanaoruhusiwa kupiga kura katika kituo cha kupigia kura.

Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa kila kituo litakuwa na idadi ya wapiga kura itakayoelekezwa na Tume na litaonesha taarifa zifuatazo kwa kila mpiga kura:-

(a) Jina kamili la mpiga kura.

(b) Jinsi.

(c) Tarehe na mwaka wa kuzaliwa.

(d) Picha ya mpiga kura.

(e) Namba ya mpiga kura.

### 3.2. Mpiga Kura Kutambua Kituo chake cha Kupigia Kura

Orodha ya wapiga kura kwa kila kituo itabandikwa siku nane (8) kabla ya Siku ya Uchaguzi ili wapiga kura walioandikishwa wapate fursa ya kutambua vituo watakavyopigia kura. Vilevile, Tume imeandaa utaratibu utakaomuwezesha mpiga kura kukagua taarifa zake zilizomo kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na kutambua kituo atakachopigia kura.

Mpiga kura anaweza kujua kituo chake cha kupigia kura kwa kufuata utaratibu ufuatao:-

1. Kuhakiki kwa kutumia mfumo wa *Voters' Interaction System* (VIS) ambapo mpiga kura atafanya yafuatayo:-

   (i) Atabofya namba *152*00#.

   (ii) Atachagua namba 9 (Uchaguzi Mkuu).

(iii) Atachagua namba 1 (Uhakiki wa taarifa za mpiga kura).

(iv) Ataingiza namba ya kadi ya mpiga kura bila kuweka herufi "T" wala alama "**-** ".

(v) Ataona ujumbe unaosomeka "ombi lako limepokelewa na linashughulikiwa, utajulishwa kwa ujumbe mfupi (SMS) hivi punde".

(vi) Atapokea ujumbe mfupi utakaonesha taarifa zake na kituo cha kupigia kura.

2. Kuhakiki kwa kupitia kituo cha huduma kwa wapiga kura (*Call Centre*) ambapo wapiga kura watapaswa kupiga simu Na. 0800112100 na kupata usaidizi wa kuhakiki taarifa zao.

3. Kuhakiki kwa kutumia tovuti ya Tume ambayo ni *www.nec.go.tz* ambapo mpiga kura atafanya yafuatayo:-

(i) Ataona sehemu iliyoandikwa"Uhakiki".

(ii) Atabofya sehemu iliyoandikwa "mfumo wa uhakiki taarifa za mpiga kura".

(iii) Itatokea sehemu iliyoandikwa ingiza namba ya mpiga kura na ataingiza namba yake kama ilivyoandikwa kwenye kadi ya mpiga kura. Kwa mfano T-1400-0073-149-0.

(iv) Akikamilisha atabofya sehemu iliyoandikwa "tafuta" na taarifa zake zitaonekana.

# SURA YA NNE

## UTEUZI WA WAGOMBEA WA KITI CHA RAIS NA MAKAMU WA RAIS

### 4.1. Siku ya Uteuzi

Kwa mujibu wa kifungu cha 32 (1), (2) na (3) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, siku ya uteuzi ni siku itakayotangazwa na Tume kuwa ndiyo siku ambayo wagombea watawasilisha Fomu za Uteuzi Tume. Fomu hizo sharti ziwasilishwe si zaidi ya saa kumi kamili (10:00) jioni siku ya uteuzi. Mkurugenzi wa Uchaguzi anatakiwa kuwepo ofisini kuanzia saa moja na nusu (1:30) asubuhi hadi saa kumi kamili (10:00) jioni. Uteuzi wa wagombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais utafanywa na Tume.

### 4.2. Sifa za Mgombea wa Kiti cha Rais na Makamu wa Rais

Kwa mujibu wa ibara ya 39(1) na 47(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, sifa za mgombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais ni zifuatavyo:-

(i) Awe raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano kwa mujibu wa sheria ya uraia;

(ii) Awe ametimiza umri wa miaka arobaini;

(iii) Awe ni mwanachama na mgombea aliyependekezwa na chama cha siasa;

(iv) Awe na sifa za kumwezesha kuwa Mbunge au Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi; na

(v) Katika kipindi cha miaka mitano kabla ya Uchaguzi Mkuu awe hajawahi kutiwa hatiani katika Mahakama yoyote kwa kosa lolote la kukwepa kulipa kodi yoyote ya Serikali.

### 4.3. Masharti ya Uteuzi wa Wagombea wa Kiti cha Rais na Makamu wa Rais

(i) Awe amedhaminiwa na wapiga kura wasiopungua mia mbili (200) waliojiandikisha kupiga kura katika kila mkoa kwa mikoa kumi na kati ya hiyo angalau mikoa miwili iwe ya Tanzania Zanzibar. **Hii inamaanisha mgombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais anatakiwa kudhaminiwa na jumla ya wapiga kura wasiopungua 2000 kutoka mikoa 10.**

(ii) Awe ameweka dhamana ya Shilingi milioni moja (1,000,000/=) kwa Tume kupitia akaunti ya amana atakayopatiwa na Mkurugenzi wa Uchaguzi siku ya kuchukua fomu za uteuzi. Mgombea akishalipia atawasilisha ***pay-in slip*** ya benki kwa Mkurugenzi wa Uchaguzi ili apatiwe stakabadhi ya kukiri mapokezi.

(iii) Awe ametoa Tamko mbele ya Jaji kwamba anazo sifa zinazotakiwa na hajapoteza sifa hizo.

### 4.4. Masharti ya Urejeshaji wa Dhamana za Wagombea

Mgombea wa kiti cha Rais atarejeshewa dhamana aliyotoa ikiwa atakidhi masharti yaliyowekwa kwa mujibu wa Sheria na Maelekezo ya Tume. Dhamana za wagombea hurejeshwa baada ya kukamilika kwa zoezi la uchaguzi husika kwa utaratibu ufuatao:-

(i) Endapo mgombea atakuwa amepata moja ya kumi (1/10) au zaidi ya kura zote halali zilizohesabiwa.

(ii) Endapo mgombea amefariki kabla ya Siku ya Uchaguzi, dhamana hiyo itarejeshwa kwa msimamizi wa mirathi anayetambulika kisheria.

Dhamana hiyo itakuwa mali ya Serikali ikiwa: -

(a) Mgombea atajitoa baada ya siku ya uteuzi; au

(b) Kura alizopata mgombea katika uchaguzi ni pungufu ya moja ya kumi (1/10) ya kura zote halali zilizohesabiwa

### 4.5. Fomu za Uteuzi (Fomu Na. 8A)

Fomu za uteuzi zitatolewa na Tume kwa mgombea aliyetambulishwa na chama cha siasa chenye usajili wa kudumu.

Fomu ya uteuzi ya mgombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais (Fomu Na. 8A) itaonesha:-

(i) Maelezo binafsi ya mtu anayeomba kugombea kiti cha Rais na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(ii) Tamko la mgombea kuwa anazo sifa za kugombea kiti cha Rais na Makamu wa Rais;

(iii) Uthibitisho wa Katibu Mkuu wa chama cha siasa kumpendekeza mgombea;

(iv) Wapiga kura wanaowadhamini wagombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais;

(v) Tamko la kisheria la mgombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(vi) Uthibitisho kwamba mgombea ameweka dhamana ya shilingi milioni moja (1,000,000/=); na

(vii) Uthibitisho wa Tume wa kumteua mgombea.

**4.6. Wadhamini wa Wagombea**

Watakaowadhamini wagombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais ni wale ambao: -

(i) Wamejiandikisha kuwa wapiga kura katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura katika mikoa husika;

(ii) Hawajamdhamini mgombea mwingine yeyote wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais; na

(iii) Wamewadhamini wagombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais kwa kutumia fomu ya uteuzi.

**Angalizo:**

Wadhamini wa wagombea si lazima wawe wanachama wa chama cha siasa kilichompendekeza mgombea na wala si lazima wawe wanachama wa chama chochote cha siasa.

**4.7. Msimamizi wa Uchaguzi Kuthibitisha Wadhamini wa Mgombea**

Wagombea au wadhamini wao watawasilisha fomu zao kwa Wasimamizi wa Uchaguzi wa jimbo ili watoe uthibitisho wa wadhamini. Hivyo, Tume inamwelekeza Msimamizi wa Uchaguzi katika kila jimbo ambalo wadhamini wametoka kutoa uthibitisho wa wadhamini hao kwa kujaza sehemu husika katika Fomu Na. 8A kwa kuweka jina kamili, saini na muhuri wa Msimamizi wa Uchaguzi.

**4.8. Uwasilishaji wa Fomu Siku ya Uteuzi**

(i) Wagombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais watawasilisha rasmi nakala nne (4) za fomu zao moja kwa moja Tume. Tume ikishapokea fomu za uteuzi na kujiridhisha kuwa wagombea wanazo sifa za kugombea itawateua.

(ii) Wagombea watawasilisha picha nne za rangi zenye ukubwa sawa na picha zinazotumika kwenye pasi ya kusafiria (*passport size*) zilizopigwa ndani ya miezi mitatu kabla ya siku ya uteuzi. Muonekano wa picha kwa nyuma uwe wa rangi nyeupe (*white background*) na nyuma ya picha liandikwe jina kamili la mgombea na chama anachokiwakilisha.

(iii) Wagombea watawasilisha stakabadhi ya malipo dhamana ya kiasi cha shilingi milioni moja (1,000,000/=) za kitanzania atakayopewa kutoka Tume.

(iv) Baada ya kuwasilisha fomu ya uteuzi, wagombea watatakiwa kutoa tamko la kuheshimu na kutekeleza Maadili ya Uchaguzi mbele ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kutumia Fomu Na. 10.

(v) Tume itabandika nakala moja ya Fomu ya Uteuzi (Fomu Na. 8A) yenye picha ya mgombea, stakabadhi ya malipo na Tamko la kuheshimu na kutekeleza Maadili ya Uchaguzi (Fomu Na. 10) kwa wagombea walioteuliwa si zaidi ya saa kumi (10:00) jioni siku ya uteuzi ili ziweze kukaguliwa na iwapo kuna pingamizi liwasilishwe Tume kupitia Fomu Na. 9A.

(vi) Mgombea akitaka anaweza kuwasilisha fomu zake Tume kuanzia siku tatu (3) kabla ya siku ya uteuzi kwa ajili ya ukaguzi na pale ambapo pana dosari mgombea ataelekezwa kurekebisha dosari hizo. Mgombea arudishiwe fomu zake mara baada ya kukaguliwa. Hata hivyo, uteuzi rasmi utafanywa siku iliyotangazwa na Tume, siku ambayo Tume itapaswa kupokea fomu husika kutoka kwa wagombea na kufanya uteuzi.

**Angalizo:** Mgombea akiwasilisha picha (*passport size*) isiyo na muonekano wa rangi nyeupe (*white background*) ateuliwe. Hii haitakuwa sababu ya pingamizi kwa mujibu wa sheria.

## 4.9. Pingamizi Dhidi ya Uteuzi wa Mgombea wa Kiti cha Rais na Makamu wa Rais

Pingamizi dhidi ya uteuzi wa mgombea linalenga kuweka zuio kwa mgombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais aliyeteuliwa na Tume kwamba hana sifa za kuteuliwa kwa mujibu wa sheria.

**(i) Wanaoruhusiwa Kuweka Pingamizi**

Kwa mujibu kanuni ya 39 ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Ubunge za mwaka 2020, wanaoruhusiwa kuweka pingamizi ni wafuatao: -

(a) Mgombea yeyote wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais;

(b) Mkurugenzi wa Uchaguzi;

(c) Mwanasheria Mkuu wa Serikali; na

(d) Msajili wa Vyama vya Siasa.

Viongozi wa vyama vya siasa vilivyowapendekeza wagombea au mtu mwingine yeyote hana haki kisheria ya kuweka pingamizi.

**(ii) Muda wa Kuweka Pingamizi**

Kwa mujibu wa kanuni ya 39 (3) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2020, muda wa kuweka pingamizi ni kuanzia saa kumi kamili (10:00) jioni ya siku ya uteuzi mpaka saa kumi kamili (10:00) jioni ya siku inayofuata baada ya siku ya uteuzi. Pingamizi zitawekwa kwa kujaza Fomu Na. 9A.

Aidha, Msajili wa Vyama vya Siasa anaruhusiwa kuweka pingamizi kuhusu masuala yanayohusu gharama za uchaguzi si chini ya siku saba (7) na si zaidi ya siku 14 baada ya siku ya uteuzi.

**(iii) Sababu za Pingamizi**

Sababu ya pingamizi inaweza kuwa yoyote kati ya zifuatazo, kwamba mgombea:-

(a) Si raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano;

(b) Hajatimiza umri wa miaka arobaini;

(c) Hana sifa za kuwa mgombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais;

(d) Hana sifa za kuwa Mbunge au Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi;

(e) Si mwanachama wa chama cha siasa kilichosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa;

(f) Hakudhaminiwa na chama cha siasa kugombea kiti cha Rais na Makamu wa Rais;

(g) Ametiwa hatiani na Mahakama yoyote kwa kosa lolote la kukwepa kulipa kodi yoyote ya Serikali katika kipindi cha miaka mitano (5) kabla ya uchaguzi;

(h) Hakudhaminiwa na wapiga kura walioandikishwa katika mikoa kumi (10) ya Jamhuri ya Muungano, ikiwemo angalau mikoa miwili (2) ya Tanzania Zanzibar;

(i) Hakudhaminiwa na idadi ya wapiga kura inayotakiwa;

(j) Hakulipa dhamana ya shilingi milioni moja (1,000,000/=) za kitanzania;

(k) Hajaambatisha picha kwenye fomu za uteuzi;

(l) Hakutoa tamko la kisheria kwa mujibu wa kifungu cha 38 (4)(a) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343;

(m) Hakutaja gharama na vyanzo vya fedha atakazotumia katika uchaguzi chini ya Sheria ya Gharama za Uchaguzi, Sura ya 278. (**Pingamizi kuhusiana na sababu hii litawekwa na Msajili wa Vyama Vya Siasa tu**);

(n) Hakurudisha fomu za uteuzi kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa na Sheria;

(o) Hajatoa tamko la kuheshimu na kutekeleza Maadili ya Uchaguzi ya mwaka 2020; na

(p) Ametenda vitendo vilivyokatazwa chini ya Sheria ya Gharama za Uchaguzi, Sura ya 278. (**Pingamizi kuhusiana na sababu hii litawekwa na Msajili wa Vyama Vya Siasa tu**).

Pingamizi lolote ni lazima liwekwe kwa maandishi kwa kutumia Fomu Na. 9A, na lazima litiwe saini na anayeweka pingamizi.

### 4.10. Uamuzi wa Tume

Baada ya kupokea pingamizi, Tume itamjulisha kwa maandishi mgombea aliyewekewa pingamizi na kumtaka atoe maelezo yake. Baada ya kupokea maelezo, Tume itatoa uamuzi wa kukubali au kukataa pingamizi husika na itawataarifu wahusika uamuzi kuhusu pingamizi hilo.

**Uamuzi wa Tume kuhusu pingamizi dhidi ya mgombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais utakuwa wa mwisho.**

### 4.11. Kutokuwepo au Kufariki kwa Mgombea

Kwa mujibu wa kifungu cha 35A cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, ikiwa baada ya saa kumi kamili (10:00) jioni siku ya uteuzi hakuna mgombea aliyeteuliwa kwa kiti cha Rais na Makamu wa Rais au katika muda wowote baada ya saa kumi kamili (10:00) jioni siku ya uteuzi na

kabla matokeo ya uchaguzi hayajatangazwa mgombea yeyote wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais atafariki, Tume itatangaza tarehe nyingine ya uteuzi kwa mujibu wa sheria.

### 4.12 . Mgombea Pekee wa Kiti cha Rais

Kwa mujibu wa kifungu 34 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura 343 iwapo mgombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais aliyeteuliwa ni mmoja: -

(i) Tume itatangaza kuwa kuna mgombea pekee wa kiti cha Rais.

(ii) Tume itawasilisha jina lake kwa wananchi kwa ajili ya kupigiwa kura na itachukuliwa kuwa amechaguliwa endapo atapata zaidi ya asilimia 50 ya kura zote zilizopigwa.

(iii) Endapo mgombea huyo atashindwa kupata zaidi ya asilimia 50, Tume itapanga tarehe nyingine kwa ajili ya Uchaguzi wa Rais.

### 4.13. Kujitoa kwa Mgombea

Kwa mujibu wa kifungu cha 35 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, mgombea wa kiti cha Rais anaweza kujitoa kugombea kwa kuwasilisha Tume yeye mwenyewe barua ya kujitoa.

Endapo mgombea atajitoa baada ya muda uliowekwa kisheria atapoteza dhamana ya fedha alizoweka kwa Mkurugenzi wa Uchaguzi.

# SURA YA TANO

## UTEUZI WA WAGOMBEA UBUNGE

### 5.1. Siku ya Uteuzi

Siku ya uteuzi ni siku itakayotangazwa na Tume kuwa ndiyo siku ambayo wagombea watawasilisha fomu za uteuzi kwa Msimamizi wa Uchaguzi, kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 37 (1) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343. Fomu hizo sharti ziwasilishwe si zaidi ya saa kumi kamili (10:00) jioni siku ya uteuzi. Msimamizi wa Uchaguzi anatakiwa awepo ofisini kuanzia saa moja na nusu (1:30) asubuhi hadi saa kumi kamili (10:00) jioni siku ya uteuzi ili kukamilisha zoezi hilo.

**Angalizo:**

Kitendo cha Wasimamizi wa Uchaguzi kutokuwepo ofisini siku ya uteuzi kinaweza kusababisha matokeo ya uchaguzi kubatilishwa. Endapo itabainika Msimamizi wa Uchaguzi ameshindwa kuwajibika ipasavyo atachukuliwa hatua kwa mujibu wa kifungu cha 89A 89B na 89C cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343.

### 5.2. Sifa za Mgombea Ubunge

Kwa mujibu wa ibara ya 67 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, mtu yeyote atakuwa na sifa za kustahili kuchaguliwa au kuteuliwa kuwa Mbunge endapo: -

(i) Ni raia wa Jamhuri ya Muungano;

(ii) Ametimiza umri wa miaka ishirini na moja (21);

(iii) Anajua kusoma na kuandika katika Kiswahili au Kiingereza;

(iv) Ni mwanachama na ni mgombea aliyependekezwa na chama cha siasa; na

(v) Hajawahi kutiwa hatiani na Mahakama yoyote kwa kosa lolote la kukwepa kulipa kodi yoyote ya Serikali katika kipindi cha miaka mitano kabla ya tarehe ya uchaguzi.

### 5.3. Kukosa Sifa za Kugombea Ubunge

Ibara ya 67 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, inaelekeza kuwa mtu hataruhusiwa kugombea Ubunge ikiwa:-

(i) Ni raia wa nchi nyingine;

(ii) Kwa mujibu wa Sheria inayotumika katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imethibitishwa rasmi kwamba mtu huyo ana ugonjwa wa akili;

(iii) Amehukumiwa na Mahakama yoyote katika Jamhuri ya Muungano na kupewa adhabu ya kifo au ya kufungwa gerezani kwa muda unaozidi miezi sita kwa kukutwa na hatia ya kosa lolote, vyovyote linavyoitwa, linaloambatana na utovu wa uaminifu;

(iv) Katika kipindi cha miaka mitano kabla ya tarehe ya Uchaguzi Mkuu amehukumiwa na kupewa adhabu ya kifungo kwa kosa linaloambatana na utovu wa uaminifu au kwa kuvunja Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma;

(v) Mtu huyo si mwanachama wa chama cha siasa na ambaye hajapendekezwa na chama cha siasa kuwa mgombea;

(vi) Mtu huyo ana maslahi yoyote katika mkataba wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano au Serikali ya Mapinduzi Zanzibar wa aina yoyote aliyowekewa miiko maalum kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Bunge, na iwapo amekiuka miiko hiyo;

(vii) Ameshika madaraka ya Afisa Mwandamizi katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, isipokuwa madaraka ambayo Rais aweza au anatakiwa kukabidhi kwa Mbunge kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano au Sheria iliyotungwa na Bunge;

(viii) Kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Bunge inayoshughulikia makosa yanayohusika na uchaguzi wa aina yoyote, mtu huyo amezuiliwa kujiandikisha kama mpiga kura au kupiga kura katika uchaguzi wa Wabunge; na

(ix) Ni mgombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Angalizo:**

1. Mtu aliyepewa adhabu ya kulipa faini au kifungo na akalipa faini hazuiwi kugombea Ubunge. Iwapo atapewa adhabu ya kulipa faini akashindwa na akatumikia kifungo na kukimaliza kabla ya siku ya uteuzi anaruhusiwa kugombea. Hii ni kwa mujibu wa Ibara ya 67 (7)(a) na (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, 1977.
2. Kiongozi wa chama cha siasa haruhusiwi kupendekeza jina lake na kujidhamini mwenyewe.

**5.4. Masharti ya Uteuzi wa Mgombea Ubunge**

**Masharti ya uteuzi wa Wagombea Ubunge ni kama ifuatavyo:-**

(i) Adhaminiwe na wapiga kura wasiopungua ishirini na tano (25) walioandikishwa kuwa wapiga kura katika jimbo linalohusika. Mgombea haruhusiwi kujidhamini yeye mwenyewe. Mpiga kura anatakiwa kudhamini mgombea Ubunge mmoja tu.

(ii) Awe ametoa tamko mbele ya Hakimu kuthibitisha kwamba anazo sifa zinazotakiwa kugombea Ubunge na hajapoteza sifa hizo.

(iii) Aweke dhamana ya shilingi elfu hamsini (50,000/=) kwa Msimamizi wa Uchaguzi kupitia akaunti ya amana ya halmashauri atakayopatiwa siku akichukua fomu za uteuzi. Mgombea akishalipa atawasilisha ***pay-in slip*** ya benki kwa Msimamizi wa Uchaguzi ili apewe stakabadhi ya kukiri mapokezi.

**Angalizo**: Ni muhimu kuhakikisha wagombea wanapewa akaunti namba ya amana ya halmashauri kwa ajili ya malipo ya dhamana wanapochukua fomu za uteuzi.

**5.5. Dhamana za Wagombea**

(i) Dhamana ya mgombea itarejeshwa baada ya uchaguzi endapo mgombea atakuwa amepata moja ya kumi (1/10) au zaidi ya kura zote halali zilizohesabiwa.

(ii) Mgombea akifariki kabla ya Siku ya Uchaguzi dhamana itarejeshwa kwa msimamizi wa mirathi anayetambulika kisheria.

Dhamana hiyo itakuwa mali ya Serikali ikiwa: -

(a) Mgombea atajitoa baada ya siku ya uteuzi; au
(b) Kura alizopata mgombea katika uchaguzi ni pungufu ya moja ya kumi (1/10) ya kura zote halali zilizohesabiwa.

**Angalizo:**

Msimamizi wa Uchaguzi haruhusiwi kuzitumia fedha za dhamana kinyume na maelekezo yaliyotolewa. Fedha ambazo hazikurudishwa kwa wagombea zitumwe Tume mara baada ya Uchaguzi.

### 5.6. Fomu ya Uteuzi (Fomu Na. 8B)

Kwa mujibu wa kifungu cha 38 (3) na (4) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 fomu ya uteuzi wa mgombea Ubunge inajumuisha mambo yafuatayo:-

(i) Maelezo binafsi ya mgombea Ubunge;

(ii) Tamko la mgombea Ubunge kwamba anazo sifa za kugombea;

(iii) Uthibitisho wa Katibu wa chama cha siasa ngazi ya mkoa, wilaya au jimbo wa kumteua mgombea;

(iv) Wapiga kura wanaomdhamini mgombea Ubunge;

(v) Tamko la kisheria la mgombea Ubunge;

(vi) Uthibitisho kwamba mgombea ameweka dhamana ya shilingi elfu hamsini (50,000/=); na

(vii) Uthibitisho wa Msimamizi wa Uchaguzi wa kumteua mgombea.

### 5.7. Utoaji wa Fomu za Uteuzi

Fomu za uteuzi zitatolewa na Wasimamizi wa Uchaguzi kwa wagombea ambao wana ushahidi wa maandishi kutoka kwa Katibu wa chama cha siasa ngazi ya mkoa, wilaya au jimbo kwamba wamependekezwa na vyama vyao kugombea.

Kila mgombea mwenye ushahidi huo apewe nakala nne (4) za Fomu za Uteuzi Na. 8B na Fomu Na. 10 ya Tamko la kuheshimu na kutekeleza Maadili ya Uchaguzi ya mwaka 2020. Fomu hizo zitolewe kwa mgombea mmoja tu anayependekezwa kutoka katika kila chama.

### 5.8. Uwasilishaji wa Fomu Siku ya Uteuzi

Mgombea awasilishe nakala nne (4) za fomu za uteuzi kwa Msimamizi wa Uchaguzi si zaidi ya saa kumi kamili (10:00) jioni siku ya uteuzi. Fomu hizo ziwasilishwe pamoja na:-

(i) Picha nne za rangi zenye ukubwa sawa na picha zinazotumika kwenye pasi ya kusafiria (*passport size*) zilizopigwa ndani ya miezi

mitatu kabla ya siku ya uteuzi. Muonekano wa picha kwa nyuma uwe wa rangi nyeupe (*white background*) na nyuma ya picha hizo liandikwe jina kamili la mgombea, jimbo na chama.

(ii) Stakabadhi ya malipo ya dhamana ya shilingi elfu hamsini (50,000/=).

(iii) Fomu Na. 10 ya tamko la kuheshimu na kutekeleza Maadili ya Uchaguzi.

Wagombea wasisitizwe kuwasilisha fomu za uteuzi wao wenyewe ili watimize sharti la kutoa tamko la kuheshimu na kutekeleza Maadili ya Uchaguzi mbele ya Msimamizi wa Uchaguzi. Aidha, wasisitizwe kuwasilisha fomu hizo mapema siku ya uteuzi ili upatikane muda wa kutosha wa kuzishughulikia.

Mgombea akitaka anaweza kuwasilisha fomu zake kuanzia siku tatu (3) kabla ya siku ya uteuzi ili Msimamizi wa Uchaguzi aweze kuzikagua na pale ambapo pana dosari amwelekeze mgombea akarekebishe dosari hizo. **Mgombea ahakikishe anarudishiwa fomu zake mara baada ya kukaguliwa.** Hata hivyo, uteuzi rasmi utafanywa siku iliyotangazwa na Tume ambapo Msimamizi wa Uchaguzi atapaswa kupokea fomu husika kutoka kwa wagombea na kufanya uteuzi.

Fomu za wagombea ambao vyama vyao vya siasa vina migogoro katika kuteua mgombea lazima zisainiwe na uongozi wa kitaifa unaotambuliwa na Msajili wa Vyama vya Siasa.

### 5.9. Utaratibu wa Kushughulikia Fomu za Uteuzi

Msimamizi wa Uchaguzi ahakikishe kwamba: -

(i) Kila fomu ya uteuzi ina majina ya wadhamini wasiopungua ishirini na tano (25) waliojaza majina yao, anuani za makazi wanapoishi, namba zao za kadi ya mpiga kura na kila mmoja awe ameweka saini yake au alama ya dole gumba.

(ii) Wadhamini wote wawe wameandikishwa kuwa wapiga kura katika jimbo husika.

(iii) Kuna uthibitisho wa maandishi kutoka kwa Katibu wa chama kilichompendekeza mgombea ngazi ya mkoa, wilaya au jimbo.

(iv) Mgombea amewasilisha picha nne (4) za rangi zenye ukubwa sawa na picha inayotumika katika pasi ya kusafiria (*passport size*). Muonekano wa picha kwa nyuma uwe wa rangi nyeupe (*white background*) na ziwe zimepigwa katika muda usiozidi miezi mitatu kabla ya siku ya uteuzi.

(v) Nyuma ya picha limeandikwa jina kamili la mgombea, jimbo na chama husika. Kama mgombea mwenyewe hakuandika jina na chama chake nyuma ya picha Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ajaze taarifa hizo na kuziweka pamoja na fomu ya uteuzi kabla ya kuipeleka Tume. Jambo hili ni muhimu ili kuepuka picha ya mgombea "X" isipewe jina la mgombea "Y" katika karatasi za kura.

(vi) Kati ya nakala nne (4) za fomu zitakazowasilishwa na mgombea kwa Msimamizi wa Uchaguzi, nakala mbili zipelekwe Tume, nakala moja ibaki kwa Msimamizi wa Uchaguzi na nakala moja irudishwe kwa mgombea. Hii itazihusu pia picha za mgombea zinazopaswa kuwasilishwa pamoja na fomu hizo.

(vii) Anabandika nakala moja ya fomu ya uteuzi (Fomu Na. 8B) yenye picha ya mgombea, stakabadhi ya malipo na Tamko la kuheshimu na kutekeleza Maadili ya Uchaguzi (Fomu Na. 10) kwa kila mgombea aliyemteua. Hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 38 (8) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kanuni ya 29 ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2020.

Fomu hizo na stakabadhi zibandikwe mahali pa wazi nje ya ofisi ya Msimamizi wa Uchaguzi saa kumi kamili (10:00) jioni siku ya uteuzi au kabla ya muda huo hadi saa kumi kamili (10:00) jioni ya siku inayofuata.

Ni vema iwepo hali ya usalama wa kutosha mahali zinapobandikwa fomu hizo ili zisiharibiwe au kuondolewa kabla ya muda ulioainishwa.

**Angalizo:**

1. Wagombea wasisitizwe kuwasilisha picha nzuri zenye muonekano mweupe kwa nyuma (*white backgraoud*).
2. Mgombea akiwasilisha picha (*passport size*) isiyo na muonekano wa rangi nyeupe (*white background*) ateuliwe. Hii haitakuwa sababu ya pingamizi kwa mujibu wa sheria.

### 5.10. Mpiga Kura Aliyedhamini Zaidi ya Mgombea Mmoja

Kifungu cha 38 (9) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 kinakataza mpiga kura kudhamini zaidi ya mgombea mmoja katika uchaguzi husika.

Kifungu cha 38 (10) cha Sheria tajwa kinaeleza kuwa endapo mpiga kura atadhamini mgombea zaidi ya mmoja na wagombea hao wakateuliwa na

Msimamizi wa Uchaguzi, udhamini huo hautabatilisha uteuzi wao, isipokuwa itakuwa ni kosa kwa mpiga kura huyo kwa mujibu wa kifungu cha 38 (11) cha sheria husika.

Utaratibu wa kushughulikia mpiga kura aliyedhamini zaidi ya mgombea mmoja utakuwa kama ifuatavyo: -

(i) Kwa mujibu wa kifungu cha 38 (11) na (12) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, mpiga kura aliyedhamini mgombea zaidi ya mmoja akikubali kosa kwa maandishi, Msimamizi wa Uchaguzi anaweza kutoa adhabu ya faini isiyozidi shilingi laki mbili (200,000/=);

(ii) Msimamizi wa Uchaguzi anatakiwa atoe stakabadhi ya malipo baada ya mdhamini kulipa fedha hizo; na

(iii) Mpiga kura asipokubali kosa kwa maandishi shauri hili litapelekwa Mahakamani.

### 5.11. Pingamizi Dhidi ya Uteuzi wa Mgombea Ubunge

Pingamizi dhidi ya uteuzi wa mgombea linalenga kuweka zuio kwa mgombea ubunge aliyeteuliwa na Msimamizi wa Uchaguzi kwamba hana sifa za kuteuliwa kwa mujibu wa sheria. Pingamizi linaweza kuwekwa kuanzia saa kumi kamili (10:00) jioni siku ya uteuzi hadi saa kumi kamili (10:00) jioni siku inayofuatia baada ya siku ya uteuzi.

**(i) Sababu za Pingamizi**

Kwa mujibu wa kifungu cha 40 (1) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 sababu ya pingamizi inaweza kuwa yoyote kati ya zifuatazo, kwamba mgombea:-

(a) Si raia wa Tanzania;

(b) Hajatimiza umri wa miaka ishirini na moja (21);

(c) Hana sifa za kuwa mgombea Ubunge;

(d) Hawezi kusoma na kuandika katika Kiswahili au Kiingereza;

(e) Si mwanachama wa chama cha siasa kilichosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa;

(f) Hakudhaminiwa na chama cha siasa kugombea Ubunge;

(g) Ametiwa hatiani kwa kosa lolote la kukwepa kulipa kodi yoyote ya Serikali katika kipindi cha miaka mitano kabla ya tarehe ya uchaguzi;

(h) Hakudhaminiwa na idadi ya wapiga kura inayotakiwa;

(i) Hakulipa dhamana ya shilingi elfu hamsini (50,000/=);

(j) Hajaambatisha picha katika fomu ya uteuzi;

(k) Hakuwasilisha tamko la kisheria;

(l) Hakutaja gharama na vyanzo vya fedha atakazotumia katika uchaguzi chini ya Sheria ya Gharama za Uchaguzi, Sura ya 278. (**Pingamizi kuhusiana na sababu hii litawekwa na Msajili wa Vyama Vya Siasa tu**);

(m) Hajatoa Tamko la kuheshimu na kutekeleza Maadili ya Uchaguzi ya mwaka 2020;

(n) Hakurudisha fomu za uteuzi kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa na sheria;

(o) Ametenda vitendo alivyokatazwa chini ya Sheria ya Gharama za Uchaguzi, Sura ya 278 (**Pingamizi kuhusiana na sababu hii litawekwa na Msajili wa Vyama vya Siasa tu**); na

(p) Hakudhaminiwa na wapiga kura walioandikishwa katika jimbo.

**(ii) Wanaoruhusiwa Kuweka Pingamizi Dhidi ya Mgombea Ubunge**

Kwa mujibu wa kifungu cha 40 (3) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 wanaoruhusiwa kuweka pingamizi ni:-

(a) Mgombea Ubunge yeyote wa jimbo linalohusika;

(b) Mkurugenzi wa Uchaguzi;

(c) Msimamizi wa Uchaguzi;

(d) Mwanasheria Mkuu wa Serikali; na

(e) Msajili wa Vyama vya Siasa.

Viongozi wa vyama vya siasa vilivyowapendekeza wagombea au mtu mwingine yeyote hana haki kisheria ya kuweka pingamizi.

**(iii) Utaratibu wa Kuweka Pingamizi Dhidi ya Mgombea Ubunge**

Pingamizi lazima liwekwe kwa maandishi kwa kutumia Fomu Na. 9B ikionesha yafuatayo:-

(a) Maelezo ya anayeweka pingamizi;

(b) Jina la mgombea aliyewekewa pingamizi;

(c) Sababu ya pingamizi;

(d) Tarehe na muda wa kuwasilisha pingamizi; na

(e) Saini ya anayeweka pingamizi.

Mgombea, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mkurugenzi wa Uchaguzi watawasilisha fomu ya pingamizi kwa Msimamizi wa Uchaguzi si zaidi ya saa kumi kamili (10:00) jioni siku inayofuatia baada ya siku ya uteuzi.

**(iv) Utaratibu wa Msajili wa Vyama vya Siasa Kuweka Pingamizi Dhidi ya Uteuzi wa Mgombea**

Msajili wa Vyama vya Siasa atawasilisha pingamizi kwa Msimamizi wa Uchaguzi kwa kutumia Fomu Na. 9B si chini ya siku saba na si zaidi ya siku 14 baada ya siku ya uteuzi.

Utaratibu wa kushughulikia pingamizi zitakazowekwa na Msajili wa Vyama vya Siasa dhidi ya mgombea utafuata utaratibu ulioelekezwa katika kipengele **5.12.**

### 5.12. Utaratibu wa Kushughulikia Pingamizi

Msimamizi wa Uchaguzi mara baada ya kupokea pingamizi, anatakiwa amtaarifu kwa maandishi mgombea aliyewekewa pingamizi juu ya pingamizi hilo na kumtaka atoe maelezo yake. Mgombea aliyewekewa pingamizi anaweza kutoa maelezo yake na kumpa Msimamizi wa Uchaguzi.

Baada ya kupata maelezo ya pande zote zinazohusika, hata kama aliyewekewa pingamizi hatatoa maelezo yake, Msimamizi wa Uchaguzi ataamua haraka iwezekanavyo kama analikubali au analikataa pingamizi hilo. Aliyeweka pingamizi na mgombea aliyewekewa pingamizi wafahamishwe kwa maandishi kuhusu uamuzi na sababu za uamuzi huo.

### 5.13. Utaratibu wa Msimamizi wa Uchaguzi Kuweka Pingamizi Dhidi ya Uteuzi wa Mgombea

Kwa mujibu wa kifungu cha 40 (5) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, pale ambapo Msimamizi wa Uchaguzi yeye mwenyewe anaweka pingamizi dhidi ya uteuzi wa mgombea, anapaswa kabla ya kuanza kufanya uchunguzi juu ya pingamizi hilo amtaarifu mgombea anayehusika kwa maandishi. Msimamizi wa Uchaguzi baada ya kukamilisha uchunguzi atawasilisha matokeo ya uchunguzi huo Tume.

### 5.14. Utaratibu wa Kukata Rufaa

Kifungu cha 40 (6) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, kinaruhusu wagombea kukata rufaa Tume kupinga uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi kuhusu pingamizi dhidi yao.

Kwa utekelezaji bora wa suala hili, Tume imeweka masharti yafuatayo: -

(i) Rufaa dhidi ya maamuzi ya Msimamizi wa Uchaguzi kuhusu uteuzi wa mgombea Ubunge zitatolewa kwa kujaza Fomu Na. 12, Tume itapeleka fomu hizo kwa Msimamizi wa Uchaguzi. Warufani watajaza nakala tatu (3) za fomu hizo.

(ii) Kwa mujibu wa kanuni ya 31 (1) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2020, fomu ziwasilishwe kwa Msimamizi wa Uchaguzi katika muda wa saa ishirini na nne (24) tangu Msimamizi wa Uchaguzi alipotoa uamuzi unaopingwa.

(iii) Msimamizi wa Uchaguzi apokee rufaa hizo kwa niaba ya Tume. Baada ya kuzipokea aandike muda wa kupokea, azisaini na kugonga muhuri wa Msimamizi wa Uchaguzi.

(iv) Msimamizi wa Uchaguzi ahakikishe kwamba: -

(a) Anaitaarifu Tume mara moja kwa njia yoyote ya haraka kuhusu kupokelewa kwa rufaa yoyote.

(b) Rufaa hizo ziwe zimeifikia Tume katika muda usiozidi siku nne (4) tangu siku ya uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi.

(c) Pamoja na rufaa hizo, awasilishe Fomu ya Uteuzi Na. 8B, Fomu ya Pingamizi Na. 9B na vielelezo vingine vinavyohusiana na rufaa hiyo.

**Angalizo:**

Rufaa yoyote itakayopokelewa na Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, lazima iwasilishwe Tume mara moja.

### 5.15. Kuwasilisha Fomu za Uteuzi Tume

Msimamizi wa Uchaguzi anatakiwa kuwasilisha nakala 2 za fomu za uteuzi Tume. Ni muhimu kuwasilisha fomu hizo mapema Tume ili kuwezesha taratibu za uchapishaji wa mfano wa karatasi za kura na karatasi za kura kufanyika mapema.

### 5.16. Kutokuwepo kwa Wagombea

Kwa mujibu wa kifungu cha 50 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, endapo baada ya uteuzi hapatakuwa na mgombea yeyote kwa sababu ya kifo, kujitoa, au sababu nyingine yoyote kama vile kutojitokeza kwa wagombea, Msimamizi wa Uchaguzi ataitaarifu Tume ili isitishe uchaguzi katika jimbo husika na kupanga tarehe nyingine ya uteuzi wa wagombea kwa mujibu wa sheria.

### 5.17. Mgombea Aliyepita Bila Kupingwa

Kwa mujibu wa kifungu cha 44 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, endapo mgombea aliyeteuliwa ni mmoja atahesabika kuwa amechaguliwa na upigaji kura hautafanyika katika jimbo hilo kwa uchaguzi wa mbunge. Aidha, Msimamizi wa Uchaguzi atamtaarifu kwa barua mgombea aliyechaguliwa baada ya muda wa pingamizi kupita. Mgombea husika atapatiwa hati ya kuchaguliwa kuwa Mbunge mara baada ya uchaguzi kukamilika.

### 5.18. Kujitoa kwa Mgombea

Kwa mujibu wa kifungu cha 48 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, mgombea anaweza kujitoa kugombea kwa kuwasilisha kwa Msimamizi wa Uchaguzi yeye mwenyewe barua ya kujitoa pamoja na tamko la kujitoa alilotoa mbele ya Hakimu. Nakala ya barua ya kujitoa ipelekwe tawi la chama kilichomdhamini kabla ya saa kumi na mbili kamili (12:00) jioni, siku inayofuata baada ya siku ya uteuzi.

Endapo mgombea atajitoa baada ya muda uliowekwa kisheria atapoteza dhamana ya fedha alizoweka kwa Msimamizi wa Uchaguzi.

Kwa mujibu wa kanuni ya 34(2)(b) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2020 mgombea akijitoa baada ya siku ya uteuzi, chama chake hakitapata nafasi ya kuweka mgombea mwingine.

### 5.19. Kufariki kwa Mgombea

Kwa mujibu wa kifungu cha 49 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, endapo Msimamizi wa Uchaguzi atajiridhisha kuwa mgombea yeyote amefariki baada ya saa kumi kamili (10:00) jioni ya siku ya uteuzi na kabla ya muda wa mwisho wa upigaji kura, atasitisha uchaguzi katika jimbo husika na kutoa taarifa Tume ili ipange tarehe nyingine ya uteuzi wa mgombea wa chama ambacho mgombea wake amefariki.

# SURA YA SITA

## UTEUZI WA WAGOMBEA UDIWANI

### 6.1. Siku ya Uteuzi

Kwa mujibu wa kifungu cha 41 (1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, siku ya uteuzi ni siku itakayotangazwa na Tume kuwa ndiyo siku ambayo wagombea watawasilisha fomu za uteuzi kwa Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata. Fomu hizo sharti ziwasilishwe kabla ya saa kumi kamili (10:00) jioni siku ya uteuzi. Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata anatakiwa awepo ofisini kuanzia saa moja na nusu (1:30) asubuhi hadi saa kumi kamili (10:00) jioni ili kukamilisha zoezi hilo.

**Angalizo:**
Ikumbukwe kwamba kitendo cha Wasimamizi wa Uchaguzi au Wasimamizi Wasaidizi kutokuwepo ofisini siku ya uteuzi kinaweza kusababisha matokeo ya uchaguzi kubatilishwa. Endapo itabainika Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ameshindwa kuwajibika ipasavyo atachukuliwa hatua kwa mujibu wa kifungu cha 88A, 88B na 88C cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292.

### 6.2. Sifa za Mgombea Udiwani

Kwa mujibu wa kifungu cha 39 (2) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa Sura ya 292, sifa za mgombea Udiwani ni zifuatazo:-

(i) Awe raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(ii) Awe ametimiza umri wa miaka ishirini na moja (21);

(iii) Awe anajua kusoma na kuandika katika Kiswahili au Kiingereza;

(iv) Awe mkazi wa kawaida wa halmashauri anayogombea;

(v) Awe mwanachama na mgombea aliyependekezwa na chama cha siasa chenye usajili wa kudumu;

(vi) Awe na kipato halali kinachomwezesha kuishi; na

(vii) Awe hajatiwa hatiani na Mahakama yoyote kwa kosa lolote la kukwepa kulipa kodi yoyote ya Serikali katika kipindi cha miaka mitano kabla ya tarehe ya uchaguzi.

### 6.3. Kukosa Sifa za Kugombea Udiwani

Kwa mujibu wa kifungu cha 40 (1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 mtu hataruhusiwa kugombea Udiwani ikiwa:-

(i) Ana utii wa nchi nyingine;

(ii) Amethibitika kisheria kwamba hana akili timamu;

(iii) Amehukumiwa kifo na Mahakama Kuu au Mahakama ya Rufaa Tanzania;

(iv) Anatumikia kifungo cha zaidi ya miezi sita gerezani kilichotolewa na Mahakama yoyote Tanzania;

(v) Yuko uhamishoni kwa zaidi ya miezi sita kwa mujibu wa Sheria ya Uhamishoni (*Deportation Act, cap 380*);

(vi) Amezuiwa na Sheria yoyote nchini kujiandikisha kuwa mpiga kura; na

(vii) Ana maslahi katika mkataba na halmashauri au kampuni yenye mkataba na halmashauri na hajatangaza kwenye magazeti yaliyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza yanayopatikana katika halmashauri husika juu ya maslahi hayo.

**Angalizo:**

1. Kwa mujibu wa kifungu cha 40 (2) (b) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 mtu aliyepewa adhabu ya kulipa faini au kifungo na akalipa faini hazuiwi kugombea Udiwani. Iwapo atapewa adhabu ya kulipa faini akashindwa na akatumikia kifungo na kukimaliza kabla ya siku ya uteuzi anaruhusiwa kugombea.
2. Kiongozi wa chama cha siasa haruhusiwi kupendekeza jina lake na kujidhamini mwenyewe.

**6.4. Masharti ya Uteuzi wa Mgombea Udiwani**

Kwa mujibu wa kifungu cha 42 cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 ili mgombea Udiwani aweze kuteuliwa anapaswa atimize masharti yafuatayo:-

(i) Awe amedhaminiwa na wapiga kura wasiopungua kumi (10) walioandikishwa katika kata anayogombea.

(ii) Awe ametoa Tamko mbele ya Hakimu kuthibitisha kwamba anazo sifa za kugombea Udiwani na hajapoteza sifa hizo.

(iii) Awe ameweka dhamana ya shilingi elfu tano (5,000/=) kwa Msimamizi wa Uchaguzi kupitia akaunti ya amana ya halmashauri atakayopatiwa siku ya kuchukua fomu za uteuzi. Mgombea akishalipia atawasilisha ***pay-in slip*** ya benki kwa Msimamizi wa Uchaguzi ili apewe stakabadhi ya kukiri mapokezi.

**Angalizo:** Ni muhimu kuhakikisha wagombea wanapewa akaunti namba ya amana ya halmashauri kwa ajili ya malipo ya dhamana wanapochukua fomu za uteuzi.

## 6.5. Fomu ya Uteuzi ( Fomu Na. 8C)

Kwa mujibu wa kifungu cha 42 cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 fomu ya uteuzi ya mgombea Udiwani itaonesha:-

(i) Maelezo binafsi ya mgombea;

(ii) Tamko la mgombea Udiwani kwamba anazo sifa za kugombea;

(iii) Uthibitisho wa Katibu wa chama cha siasa ngazi ya wilaya, jimbo au kata wa kumpendekeza kuwa mgombea;

(iv) Tamko, majina, anuani na namba za wapiga kura wasiopungua kumi waliomdhamini mgombea;

(v) Tamko la kisheria la mgombea kuthibitisha kwamba anazo sifa zinazotakiwa kugombea Udiwani na hajapoteza sifa hizo;

(vi) Uthibitisho kuwa mgombea ameweka dhamana ya shilingi elfu tano (5,000/=); na

(vii) Uthibitisho wa Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata kumteua mgombea.

## 6.6. Utoaji wa Fomu za Uteuzi

(i) Fomu za uteuzi zitatolewa na Wasimamizi wa Uchaguzi au Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi kwa wagombea ambao wana ushahidi wa maandishi kutoka kwa Katibu wa chama cha siasa ngazi ya wilaya, jimbo au kata kwamba wamependekezwa na vyama vyao.

(ii) Kila mgombea mwenye ushahidi huo apewe nakala nne (4) za Fomu za Uteuzi Na. 8C na Fomu za Tamko la kuheshimu na kutekeleza Maadili ya Uchaguzi Na. 10. Fomu hizo zitolewe kwa mgombea mmoja tu aliyependekezwa kutoka kila chama cha siasa.

## 6.7. Uwasilishaji wa Fomu Siku ya Uteuzi.

(i) Mgombea anayependekezwa na chama cha siasa awasilishe kwa Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata kabla ya saa kumi kamili (10:00) jioni siku ya uteuzi nyaraka zifuatazo:-

(a) Nakala nne (4) za fomu ya uteuzi.

(b) Picha nne (4) za rangi zenye ukubwa sawa na picha inayotumika katika pasi ya kusafiria (*passport size*) zilizopigwa ndani ya miezi mitatu kabla ya siku ya uteuzi. Muonekano wa picha kwa nyuma uwe wa rangi nyeupe (*white background*) na nyuma ya picha liandikwe jina kamili la mgombea, kata na chama.

(c) Stakabadhi ya malipo ya dhamana ya shilingi elfu tano (5,000/=).

(ii) Mgombea anaweza kuwasilisha fomu zake kuanzia siku tatu (3) kabla ya siku ya uteuzi ili Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata aweze kuzikagua na ikiwa kuna dosari amuelekeze mgombea akarekebishe dosari hizo. **Mgombea arejeshewe fomu zake mara baada ya kukaguliwa.** Hata hivyo, uteuzi rasmi utafanyika siku iliyotangazwa na Tume, ambapo Msimamizi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata atapaswa kupokea fomu husika kutoka kwa wagombea na kufanya uteuzi.

Fomu za wagombea ambao vyama vyao vina mgogoro katika kuteua mgombea, lazima zisainiwe na uongozi unaotambuliwa na Msajili wa Vyama vya Siasa wa ngazi ya mkoa, wilaya au jimbo.

**Angalizo:**

1. Wagombea wasisitizwe kuwasilisha picha nzuri zenye muonekano mweupe kwa nyuma (*white background*).
2. Mgombea akiwasilisha picha (*passport size*) isiyo na muonekano wa rangi nyeupe (*white background*) ateuliwe. Hii haitakuwa sababu ya pingamizi kwa mujibu wa sheria.

## 6.8. Utaratibu wa Kushughulikia Fomu za Uteuzi

Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata ahakikishe kwamba:-

(i) Kila fomu ya uteuzi ina majina ya wadhamini wasiopungua kumi (10) waliojaza majina yao, anwani za makazi (wanapoishi), namba za wapiga kura na kila mmoja wao awe ameweka saini yake au alama ya dole gumba.

(ii) Wadhamini wote hao wawe wameandikishwa kuwa wapiga kura katika kata husika.

(iii) Kuna uthibitisho wa maandishi kutoka kwa Katibu wa chama kilichomteua mgombea ngazi ya wilaya, jimbo au kata.

(iv) Mgombea amewasilisha picha nne (4) za rangi zenye ukubwa sawa na picha inayotumika katika pasi ya kusafiria *(passport size)*. Muonekano wa picha kwa nyuma uwe rangi nyeupe (white background).

(v) Nyuma ya picha limeandikwa jina kamili la mgombea, kata na chama husika. Kama mgombea mwenyewe hakuandika jina na chama chake nyuma ya picha Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata ajaze taarifa hizo na kuziweka pamoja na fomu ya uteuzi kabla ya kuipeleka Tume. Jambo hili ni muhimu ili kuepuka picha ya mgombea "X" isipewe jina la mgombea "Y" katika karatasi za kura.

(vi) Kati ya nakala nne (4) za fomu zitakazowasilishwa na mgombea kwa Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata, nakala mbili zipelekwe Tume, nakala moja ibaki kwa Msimamizi wa Uchaguzi na nakala moja irudishwe kwa mgombea. Hii itahusu pia picha za mgombea zinazopaswa kuwasilishwa pamoja na fomu hizo.

(vii) Kwa mujibu wa kifungu cha 42 (8) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za mitaa, Sura ya 292 na kanuni ya 27 ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020, Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata anatakiwa kubandika nakala moja ya Fomu ya Uteuzi (Fomu Na. 8C) yenye picha ya mgombea, stakabadhi ya malipo na Tamko la kuheshimu na kutekeleza Maadili ya Uchaguzi (Fomu Na. 10) kwa kila mgombea aliyemteua.

Fomu hizo na stakabadhi zitabandikwa mahali pa wazi nje ya ofisi ya Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata saa kumi kamili (10:00) jioni siku ya uteuzi au kabla ya muda huo hadi saa kumi kamili (10:00) jioni ya siku inayofuata.

Ni vema iwepo hali ya usalama wa kutosha mahali zinapobandikwa fomu hizo ili zisiharibiwe au kuondolewa kabla ya muda ulioainishwa.

### 6.9. Mpiga Kura Anayedhamini Mgombea Udiwani Zaidi ya Mmoja

Mpiga kura atatakiwa kumdhamini mgombea udiwani mmoja tu katika uchaguzi unaohusika. Hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 42 (9) cha Sheria

ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292. Endapo atadhamini mgombea zaidi ya mmoja na wagombea hao wakateuliwa na Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata, udhamini huo hautabatilisha uteuzi wao, isipokuwa itakuwa ni kosa kwa mpiga kura huyo kwa mujibu wa kifungu cha 42 (11) cha sheria tajwa.

Kwa mujibu wa kifungu cha 42 (11) na (12) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, mpiga kura aliyedhamini mgombea zaidi ya mmoja akikubali kosa kwa maandishi, Msimamizi wa Uchaguzi anaweza kutoa adhabu ya faini isiyozidi shilingi laki mbili (200,000/=).

Msimamizi wa Uchaguzi anatakiwa atoe stakabadhi ya malipo pale mdhamini anapolipa fedha hizo.

Mpiga Kura asipokubali kosa kwa maandishi shauri litapelekwa Mahakamani.

## 6.10. Pingamizi Dhidi ya Uteuzi wa Mgombea Udiwani

Pingamizi dhidi ya uteuzi wa mgombea linalenga kuweka zuio kwa mgombea Udiwani aliyeteuliwa na Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata kwamba hana sifa za kuteuliwa kwa mujibu wa sheria.

Pingamizi linaweza kuwekwa kuanzia saa kumi kamili (10:00) jioni siku ya uteuzi hadi saa kumi kamili (10:00) jioni siku inayofuatia baada ya siku ya uteuzi.

### (i) Sababu za Pingamizi

Kwa mujibu wa kifungu cha 44(1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, sababu ya pingamizi inaweza kuwa yoyote kati ya zifuatazo, kwamba Mgombea:-

(a) Si raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(b) Hajatimiza umri wa miaka 21;

(c) Hajui kusoma na kuandika katika Kiswahili au Kiingereza;

(d) Si mwanachama wa chama cha siasa chenye usajili wa kudumu;

(e) Si mkazi wa kawaida wa halmashauri ambayo kata anayogombea imo;

(f) Ametiwa hatiani na Mahakama yoyote kwa kosa lolote la kukwepa kulipa kodi yoyote ya Serikali katika kipindi cha miaka mitano kabla ya tarehe ya uchaguzi;

(g) Hajadhaminiwa na wapiga kura walioandikishwa katika kata husika,

(h) Hajadhaminiwa na wapiga kura wasiopungua kumi (10);

(i) Hakuna uthibitisho kuwa mgombea ameweka dhamana ya shilingi elfu tano (5,000/=);

(j) Hakuwasilisha picha;

(k) Hajawasilisha Tamko la Kisheria;

(l) Hajadhaminiwa na chama cha siasa kilichosajiliwa;

(m) Hakutaja gharama na vyanzo vya fedha atakazotumia kwenye uchaguzi (**Pingamizi kuhusiana na sababu hii litawekwa na Msajili wa Vyama Vya Siasa tu**);

(n) Hajatoa Tamko la kuheshimu na kutekeleza Maadili ya Uchaguzi ya mwaka 2020;

(o) Hakurudisha fomu za uteuzi kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa na Sheria; na

(p) Ametenda vitendo vilivyokatazwa chini ya Sheria ya Gharama za Uchaguzi, Sura ya 278 (**Pingamizi kuhusiana na sababu hii litawekwa na Msajili wa Vyama vya Siasa tu**).

**(ii) Wanaoruhusiwa Kuweka Pingamizi**

(a) Mgombea Udiwani yeyote wa kata inayohusika;

(b) Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi; na

(c) Msajili wa Vyama vya Siasa.

**Angalizo:**

Viongozi wa vyama vya siasa waliowapendekeza wagombea au mtu mwingine yeyote hawana haki kisheria ya kuweka pingamizi.

**(iii) Utaratibu wa Kuweka Pingamizi**

Pingamizi ni lazima liwekwe kwa maandishi kwa kutumia Fomu Na. 9C. Fomu hizo zinapaswa kujazwa nakala mbili zikionyesha yafuatayo: -

(a) Maelezo ya anayeweka pingamizi;

(b) Jina la mgombea aliyewekewa pingamizi;

(c) Sababu za pingamizi;

(d) Tarehe na muda wa kuwasilisha pingamizi; na

(e) Saini ya aliyeweka pingamizi.

Mgombea, Msimamizi wa Uchaguzi au Mkurugenzi wa Uchaguzi atawasilisha fomu ya pingamizi kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata si zaidi ya saa kumi kamili (10:00) jioni siku inayofuatia baada ya siku ya uteuzi.

**(iv) Utaratibu wa Msajili wa Vyama vya Siasa Kuweka Pingamizi Dhidi ya Uteuzi wa Mgombea**

Msajili wa Vyama vya Siasa atawasilisha pingamizi kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata kwa kutumia Fomu Na. 9C si chini ya siku saba na si zaidi ya siku 14 baada ya siku ya uteuzi.

Utaratibu wa kushughulikia pingamizi zitakazowekwa na Msajili wa Vyama vya Siasa dhidi ya mgombea utafuata utaratibu ulioelekezwa katika kipengele cha **(v).**

**(v) Kushughulikia Pingamizi Dhidi ya Uteuzi wa Mgombea Udiwani**

(a) Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata mara baada ya kupokea pingamizi anatakiwa amtaarifu kwa maandishi mgombea aliyewekewa pingamizi kuhusu pingamizi hilo na kumtaka atoe maelezo yake. Mgombea aliyewekewa pingamizi anaweza kujibu na kumpa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata maelezo yake.

(b) Baada ya kupata taarifa za pande zote Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata aamue haraka iwezekanavyo kama analikubali au anakataa pingamizi hilo.

(c) Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata baada ya kufanya uamuzi kuhusu pingamizi awasilishe uamuzi huo kwa Msimamizi wa Uchaguzi ili aupitie na kuona kama umezingatia sheria. Msimamizi wa Uchaguzi ana mamlaka ya kubadili uamuzi huo kama atabaini kuwa haukuzingatia matakwa ya sheria.

(d) Baada ya Msimamizi wa Uchaguzi kutoa maamuzi ya kukubaliana au kukataa uamuzi wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata, Wagombea wafahamishwe kwa maandishi kuhusu uamuzi huo. Aidha, Msimamizi wa Uchaguzi kama analikubali pingamizi hilo atatakiwa kuwajulisha wagombea sababu za uamuzi wake.

> **Angalizo:**
>
> Msimamizi wa Uchaguzi ni lazima atoe uamuzi wake kuhusu kukubali au kukataa uamuzi wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata dhidi ya pingamizi kwa kujaza sehemu husika katika fomu Na. 9C.

**6.11. Utaratibu wa Kuwasilisha Rufaa.**

Kifungu cha 44 (5) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 kinaruhusu wagombea kukata rufaa Tume dhidi ya uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi kuhusu pingamizi dhidi yao.

Katika utekelezaji bora wa suala hili masharti yafuatayo yatazingatiwa:-

(i) Rufaa dhidi ya uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi kuhusu uteuzi wa mgombea Udiwani zitawasilishwa kwa kutumia Fomu Na. 12. Warufani watajaza nakala tatu (3) ya fomu hizo. Aidha, fomu husika zitapelekwa na Tume kwa Wasimamizi wa Uchaguzi.

(ii) Fomu za rufaa ziwasilishwe kwa Msimamizi wa Uchaguzi katika muda wa saa ishirini na nne (24) tangu Msimamizi wa Uchaguzi alipotoa uamuzi unaopingwa. Msimamizi wa Uchaguzi apokee rufaa hizo kwa niaba ya Tume. Hii ni kwa mujibu wa kanuni ya 29 ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020.

(iii) Msimamizi wa Uchaguzi ahakikishe kwamba:-

(a) Anaitaarifu Tume mara moja kwa njia yoyote ya haraka kuhusu kupokelewa kwa rufaa.

(b) Rufaa hizo ziwasilishwe Tume katika muda usiozidi siku nne (4) tangu siku ya kupokelewa kwa rufaa.

(c) Pamoja na rufaa hizo, awasilishe Fomu za Uteuzi Na. 8C, Fomu za Pingamizi Na. 9C na vielelezo vingine vinavyohusiana na rufaa hiyo.

> **Angalizo:**
>
> Rufaa yoyote itakayopokelewa na Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata lazima iwasilishwe Tume mapema iwezekanavyo.

**6.12. Kuwasilisha Fomu za Uteuzi Tume**

Msimamizi wa Uchaguzi anatakiwa kuwasilisha nakala 2 za fomu za uteuzi Tume. Ni muhimu kuwasilisha fomu hizo mapema, Makao Makuu ya Tume ili kuwezesha taratibu za uchapishaji wa mfano wa karatasi za kura na karatasi za kura kufanyika mapema.

### 6.13. Kutokuwepo kwa Wagombea

Kwa mujibu wa kifungu cha 52 cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, endapo baada ya uteuzi hapatakuwa na mgombea yeyote kwa sababu ya kifo, kujitoa, au sababu nyingine yoyote Msimamizi wa Uchaguzi ataitaarifu Tume ili iweze kusitisha Uchaguzi na kupanga tarehe nyingine ya uteuzi wa wagombea katika kata husika.

### 6.14. Mgombea Aliyepita bila Kupingwa

Kwa mujibu wa kifungu cha 45 (2) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, endapo mgombea aliyeteuliwa ni mmoja atahesabika kuwa amechaguliwa na upigaji kura hautafanyika katika kata hiyo kwa uchaguzi wa Diwani. Msimamizi wa Uchaguzi atamtangaza mgombea aliyechaguliwa baada ya muda wa pingamizi kupita. Mgombea husika atapatiwa hati ya kuchaguliwa kuwa Diwani mara baada ya uchaguzi kukamilika. Aidha, Msimamizi wa Uchaguzi ataitaarifu Tume kuhusu kuchaguliwa kwa mgombea husika.

### 6.15. Kujitoa kwa Mgombea

Kwa mujibu wa kifungu cha 50 cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, mgombea anaweza kujitoa kugombea kwa kuwasilisha kwa Msimamizi wa Uchaguzi yeye mwenyewe barua ya kujitoa pamoja na tamko la kujitoa alilotoa mbele ya Hakimu. Nakala ya barua ya kujitoa itapelekwa kwenye tawi la chama kilichomdhamini kabla ya saa kumi na mbili (12:00) jioni ya siku inayofuata baada ya siku ya uteuzi.

Endapo mgombea atajitoa baada ya muda wa uteuzi kupita atapoteza dhamana ya fedha alizoweka kwa Msimamizi wa Uchaguzi na chama chake hakitapata nafasi ya kuteua mgombea mwingine.

# SURA YA SABA

## UTARATIBU WA WATUMISHI WA UMMA KUGOMBEA UBUNGE NA UDIWANI

### 7.1. Wanaoruhusiwa na Wasioruhusiwa Kugombea Miongoni mwa Watumishi wa Umma

Wasimamizi wa Uchaguzi katika kutekeleza majukumu yao hususan wakati wa uteuzi wa wagombea wanatakiwa kuzingatia Waraka wa Mkuu wa Utumishi wa Umma Na. 1 wa mwaka 2015 ukisomwa pamoja na miongozo yake. Waraka huo unawataka watumishi wote wa Umma watakaopenda kugombea nyadhifa za kisiasa katika ngazi mbalimbali waruhusiwe, isipokuwa wale ambao kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hawaruhusiwi kuwa wanachama wa chama chochote cha siasa wala kujihusisha na shughuli za kisiasa zaidi ya kupiga kura.

Watumishi hao ni:-

(i) Askari wote walio kazini, Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Idara ya Uhamiaji na Zimamoto na Uokozi;

(ii) Majaji na Mahakimu wa Mahakama katika ngazi zote;

(iii) Mwenyekiti, Makamu mwenyekiti, Wajumbe na Watumishi wote wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi pamoja na Wasimamizi wa Uchaguzi; na

(iv) Vyombo vingine vya utendaji Serikalini ambavyo kwa hulka yake na kwa mujibu wa utendaji wake wa kazi, watumishi wake hawaruhusiwi kuwa wanachama wa chama chochote cha Siasa na/au kushiriki katika mambo ya Siasa. Hao ni pamoja na watumishi wote wa Ofisi ya Bunge, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Idara ya Usalama wa Taifa, Mawakili wa Serikali na Watumishi wa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa.

### 7.2. Wakati wa Kujitayarisha Kugombea

Mtumishi wa Umma atakayeamua kugombea nafasi ya uongozi wa kisiasa atatakiwa kutoa taarifa rasmi kwa maandishi kwa mamlaka iliyomuajiri na kisha ataomba na atapewa likizo bila malipo ili ashughulikie taratibu zake za kugombea nafasi aliyoomba. Utaratibu utakuwa kama ifuatavyo:-

(i) Kwa wagombea Ubunge na wagombea Udiwani, likizo hiyo itaanza tangu siku ya kuvunjwa Bunge na itakoma tarehe ya kuteuliwa na Tume kuwa mgombea.

(ii) Kwa upande wa Viti Maalum vya Ubunge na Udiwani, likizo hiyo itaanza siku ya kuvunjwa Bunge hadi tarehe ambayo Tume itamtangaza kuwa Mbunge au Diwani.

### 7.3. Baada ya Kuteuliwa au Kutangazwa na Tume

Utaratibu kwa watumishi wote wa Umma watakaogombea nyadhifa za kisiasa nchini utakuwa kama ifuatavyo: -

(i) Mtumishi wa Umma atakayeamua kugombea nafasi ya Ubunge anaruhusiwa kufanya hivyo, na baada ya Tume kumtangaza kuwa mgombea wa Ubunge, atalazimika kuacha kazi;

(ii) Mtumishi wa Umma atakayeamua kugombea Ubunge kupitia Viti Maalum, anaruhusiwa kufanya hivyo, na baada ya Tume kumtangaza kuwa Mbunge, utumishi wake utakoma; na

(iii) Mtumishi wa Umma, atakayeamua kugombea nafasi ya Udiwani anaruhusiwa kufanya hivyo na baada Tume kumtangaza kuwa Mgombea wa Udiwani, atalazimika kuacha kazi.

# SURA YA NANE

## KAMPENI ZA UCHAGUZI

### 8.1 Kipindi cha Kampeni

Kwa mujibu wa kifungu cha 46 (1) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 53 (1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 kipindi cha kampeni za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani hutangazwa na Tume. Kampeni zitaanza siku moja baada ya siku ya uteuzi na kumalizika siku moja kabla ya siku ya uchaguzi.

Kwa kuzingatia kanuni ya 40 ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2020 na kanuni ya 35 ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020 zikisomwa pamoja na kipengele cha 2.1(c) cha Maadili ya Uchaguzi ya mwaka 2020 muda wa kuanza kampeni utakuwa saa mbili kamili (2:00) asubuhi na kumalizika saa kumi na mbili kamili (12:00) jioni.

### 8.2. Wajibu wa Tume Katika Kuratibu Ratiba ya Kampeni za Wagombea wa Kiti cha Rais na Makamu wa Rais

(i) Kwa uchaguzi wa Rais, Mkurugenzi wa Uchaguzi atapaswa kabla ya kuanza kwa kampeni za uchaguzi, kuvitaka vyama vya siasa vinavyoshiriki uchaguzi wa Rais kuwasilisha ratiba za kampeni siku saba (7) kabla ya siku ya uteuzi.

(ii) Ratiba za Kampeni zitaonesha tarehe, muda, mkoa, wilaya na mahali ambapo mgombea atafanya kampeni zake. Mkurugenzi wa Uchaguzi baada ya kupokea mapendekezo ya ratiba za kampeni kutoka kwenye vyama vya siasa ataitisha mkutano kwa ajili ya kuratibu ratiba za kampeni.

(iii) Baada ya Mkurugenzi wa Uchaguzi kutayarisha ratiba ya kampeni iliyokwisharatibiwa atawapatia nakala hiyo wafuatao:-

- (a) Vyama vyote vya siasa vinavyoshiriki katika Uchaguzi wa Rais;
- (b) Waratibu wa Uchaguzi wa Mikoa;
- (c) Wakuu wa Mikoa - kwa taarifa;
- (d) Wasimamizi wa Uchaguzi; na
- (e) Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini kwa madhumuni ya kutoa ulinzi katika mikutano ya kampeni.

(iv) Endapo chama cha siasa kinakusudia kufanya marekebisho ya mahali pa kufanyia kampeni au kubadilisha ratiba, kitamfahamisha Mkurugenzi wa Uchaguzi kwa maandishi ambaye ataitisha mkutano wa vyama vyote vya siasa vinavyoshiriki uchaguzi au wagombea kukubaliana juu ya mabadiliko hayo.

(v) Endapo itaonekana ipo haja ya mabadiliko yaliyopendekezwa na kukubaliwa na mkutano wa vyama vyote vya siasa vinavyoshiriki uchaguzi, Mkurugenzi wa Uchaguzi atafanya mabadiliko hayo na kuvifahamisha vyama vya siasa vinavyoshiriki na wadau wengine waliotajwa katika kipengele (iii).

(vi) Tume ina wajibu wa kutoa maelekezo na kukemea pale inapoona taratibu za kampeni hazifuatwi kwa mujibu wa sheria na Maadili ya Uchaguzi.

## 8.3. Wajibu wa Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi katika Kuratibu Ratiba za Kampeni za Wagombea Ubunge na Udiwani

(i) Kwa uchaguzi wa Ubunge na Udiwani, Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata atapaswa kabla ya kuanza kwa kampeni za uchaguzi, kuvitaka vyama vya siasa kuwasilisha ratiba za Kampeni.

(ii) Vyama vya siasa vinapaswa kuwasilisha mapendekezo ya ratiba za kampeni kwa Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata siku saba (7) kabla ya siku ya uteuzi. Ratiba za kampeni zioneshe tarehe, muda, na mahali ambapo mgombea atafanya kampeni zake.

(iii) Baada ya Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata kupokea ratiba zote za kampeni za uchaguzi kutoka kwenye vyama vya siasa atatakiwa kuitisha mkutano wa vyama vya siasa au wagombea wanaoshiriki uchaguzi kwa ajili ya kuratibu ratiba hizo ili kuepusha mgongano wakati wa kampeni.

(iv) Baada ya Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata kutayarisha ratiba ya kampeni iliyoandaliwa na kukubaliwa atawapatia nakala wafuatao:-

   (a) Vyama vyote vya siasa vinavyoshiriki katika uchaguzi wa Ubunge au Udiwani;

   (b) Mkuu wa Wilaya - kwa taarifa;

(c) Kamanda wa Polisi wa Wilaya kwa madhumuni ya kutoa ulinzi katika mikutano ya Kampeni; na

(d) Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi ngazi ya jimbo na kata.

(v) Endapo chama cha siasa kinakusudia kufanya marekebisho ya eneo la kampeni au kubadilisha ratiba, kitamfahamisha Msimamizi wa Uchaguzi na kuainisha sababu za kutaka kufanya hivyo.

Msimamizi wa Uchaguzi ataitisha mkutano wa vyama vyote vinavyoshiriki katika uchaguzi husika ili kujadili na kukubaliana juu ya mabadiliko hayo na kisha atavipatia nakala ya ratiba yenye mabadiliko husika vyama vyote vinavyoshiriki katika uchaguzi na wadau wengine wanaotajwa katika kipengele (iv).

(vi) Ni muhimu Msimamizi wa Uchaguzi azingatie muda, umbali wa eneo moja na lingine ambapo mikutano inafanyika na barabarana zitakazotumika kufikia maeneo hayo wakati wa kupanga ratiba za kampeni. Hii itasaidia kuepusha mgongano wa wafuasi wa vyama unaoweza kujitokeza kutokana na upanagji usio mzuri wa ratiba ya kampeni utakaosababisha kuchochea vurugu na uvunjifu wa amani.

**Angalizo:**

Ratiba ya kampeni iliyowasilishwa na Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata kwa Kamanda wa Polisi wa Wilaya itakuwa ndiyo taarifa rasmi ya mikutano ya kampeni na atatakiwa kutoa ulinzi katika mikutano kwa vyama vyote vya siasa. Hivyo, vyama havipaswi kuomba vibali vyovyote vya ziada kuendesha mikutano ya kampeni za uchaguzi.

### 8.4. Wajibu wa Mgombea, Chama cha Siasa na Wakala Wakati wa Kampeni

Kwa mujibu wa kifungu cha 51 cha Sheria ya Taifa Uchaguzi, Sura ya 343 kikisomwa pamoja na kanuni ya 43 (2) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2020 na kifungu cha 53 (1) (b) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 kikisomwa pamoja na kanuni ya 36 Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020, mgombea, chama cha siasa au wakala wa mgombea ana wajibu ufuatao:-

(i) Kupanga na kuwasilisha ratiba ya kampeni kwa Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata siku saba (7) kabla ya siku ya uteuzi;

(ii) Kuendesha kampeni za mgombea; na

(iii) Kufanya kampeni za nyumba kwa nyumba.

| **Angalizo:** |
|---|
| Kampeni za nyumba kwa nyumba haziratibiwi na Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata. |

### 8.5. Maelekezo ya Jumla Kuhusu Kampeni

(i) Ni marufuku kwa mgombea, chama cha siasa au wakala, kufanya kampeni Siku ya Uchaguzi.

(ii) Mpiga kura au mtu mwingine yeyote haruhusiwi kwenda katika kituo cha kupigia kura na alama, vazi au bango linaloashiria kukipigia kampeni chama au mgombea.

(iii) Endapo vyama vya siasa au mgombea yeyote atahitaji kutumia machapisho kama vile mabango au vipeperushi vyenye matangazo ya kampeni vinapaswa kuomba idhini kwa mamlaka husika kama ifuatavyo:-

   (a) Kwa uchaguzi wa kiti cha Rais, kibali kiombwe Tume.

   (b) Kwa uchaguzi wa Ubunge au Udiwani, kibali kiombwe kwa Msimamizi wa Uchaguzi.

(iv) Tume itatoa mfano wa karatasi za kura kwa Vyama vyote vya Siasa vinavyoshiriki katika Uchaguzi ili zitumike kunadi Wagombea wao katika Kampeni za Uchaguzi.

(v) Msimamizi wa Uchaguzi atatakiwa kutoa mfano wa karatasi za kura kwa vyama vya siasa vinavyoshiriki uchaguzi katika halmashauri yake. Vyama vyote vipate idadi sawa kama itakavyoelekezwa na Tume.

| **Angalizo:** |
|---|
| Machapisho ambayo hayajaidhinishwa na mamlaka husika hayataruhusiwa kutumika katika kampeni. |

### 8.6. Maadili ya Uchaguzi

Maadili ya Uchaguzi ni makubaliano ya pamoja baina ya vyama vya siasa, Serikali na Tume yanayoeleza mambo yanayotakiwa kufanywa au kuzingatiwa na yasiyotakiwa kufanywa katika mchakato wa uchaguzi wakati wa kampeni za uchaguzi, upigaji kura na kutangaza matokeo ya uchaguzi.

Pamoja na mambo mengine, Maadili ya Uchaguzi yanahusu kuheshimiana, kuzingatia ratiba za kampeni, kuelimisha wanachama wa vyama katika misingi ya kuelewa sera za vyama husika, kutojenga chuki, kushirikiana na kutobeba silaha za aina yoyote katika mikutano.

Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata anatakiwa kutekeleza zoezi la kusimamia na kuendesha uchaguzi kwa mujibu wa sheria, kanuni, maelekezo ya Tume na kuzingatia uwazi na uadilifu. Hivyo, mnaelekezwa kuzingatia Maadili ya Uchaguzi ya mwaka 2020 kwani kushindwa kufanya hivyo kunaweza kusababisha kuharibika kwa mchakato wa uchaguzi.

Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata baada ya kupata maelekezo kutoka Tume ataunda kamati za maadili katika ngazi ya jimbo na kata. Hivyo, anatakiwa kuvitaarifu vyama vya siasa na Serikali kuwasilisha majina ya wajumbe siku saba (7) kabla ya siku ya uteuzi. Kamati hizo zitasimamia na kushughulikia malalamiko yanayotokana na ukiukwaji wa Maadili wakati wa kampeni za uchaguzi kuanzia hatua ya kuanza kwa kampeni hadi kukamilika kwa kampeni za uchaguzi.

Vyama vya siasa vinavyoshiriki uchaguzi vina wajibu wa kuhakikisha vinatekeleza makubaliano ya kuheshimu na kutekeleza maadili ya uchaguzi ili kuhakikisha kuwa kampeni zinafanyika kwa amani na utulivu.

# SURA YA TISA

## UPIGAJI KURA

### 9.1 Maandalizi Kuelekea Siku ya Upigaji Kura

Msimamizi wa Uchaguzi atapokea kutoka Tume idadi na orodha ya vituo vya kupigia kura kwa kila jimbo husika. Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 56 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 57 cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, Msimamizi wa Uchaguzi atatakiwa kufanya maandalizi ya vituo vya kupigia na maandalizi mengine muhimu mapema kabla ya siku ya upigaji kura.

### 9.2. Vituo vya Kupigia Kura

(i) Vituo vilivyotumika kuandikishia wapiga kura ndivyo vitakavyotumika kama vituo vya kupigia kura.

(ii) Idadi ya wapiga kura watakaopiga kura katika kituo itapangwa na Tume. Ikiwa wapiga kura ni wengi katika vituo vya kuandikisha wapiga kura, Tume inaweza kugawa wapiga kura katika vituo A, B, C. Kwa mfano ikipangwa idadi ya wapiga kura kwa kituo ni 450 na walioandikishwa ni wapiga kura 1300, kituo hicho kitagawanywa mara tatu, kituo A wapiga kura 450, kituo B wapiga kura 450 na kituo C wapiga kura 400.

(iii) Vituo vya kupigia kura havitakiwi kuwekwa kwenye ofisi za chama chochote cha siasa, majengo ya ibada, vituo au kambi za polisi, kambi za jeshi, nyumba za viongozi au mashabiki wa vyama vya siasa. Maeneo yenye changamoto ni vema wagombea na vyama vya siasa vijulishwe mapema.

(iv) Msimamizi wa Uchaguzi atatakiwa kuhakikisha mabango mshale yanabandikwa kwa namna ambayo yatasaidia kuonesha vituo vilipo. Kutakuwa na mabango mshale yatakayobandikwa kwenye barabara kuu na njia za kuelekea vilipo vituo vya kupigia kura.

(v) Msimamizi wa Uchaguzi atatakiwa kuvitembelea vituo vyote ili kuvikagua kuona kama vinakidhi sifa, vigezo na mahitaji kwa ajili ya kupigia kura na kuhesabu Kura. Hivyo, ni muhimu kuhakikisha kuwa vituo vina nafasi ya kutosha kwa ajili ya kupiga kura na kuhesabu kura.

(vi) Msimamizi wa Uchaguzi atavipatia vyama vya siasa orodha ya vituo vya kupigia kura siku kumi na nne (14) kabla ya Siku ya Uchaguzi.

**Angalizo**: Ikiwa kutakuwa na vituo vya kupigia kura zaidi ya kimoja katika eneo moja kwa mfano katika shule Msimamizi wa Uchaguzi ahakikishe vituo hivyo havikaribiani..

### 9.3. Tangazo la Uchaguzi (*Notice of Election*)

Tangazo la Uchaguzi linalotolewa kwa mujibu wa kifungu cha 47 (1) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 49 (1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292. Msimamizi wa Uchaguzi anatakiwa kutoa tangazo hilo siku nane (8) kabla ya siku ya uchaguzi ili kuwawezesha wapiga kura kufahamu mahali, tarehe na siku ya kupiga kura.

Tangazo hilo linatakiwa litolewe kwa ngazi ya jimbo na kata. Pia, tangazo litatolewa kwa kila kituo cha kupigia kura.

(i) Tangazo la Uchaguzi la jimbo au kata lioneshe:-

- (a) Tarehe ya upigaji kura;
- (b) Saa ya kufungua na kufunga vituo vya kupigia kura;
- (c) Sehemu ambazo waliojiandikisha kupiga kura watapiga kura; na
- (d) MFANO WA KARATASI ZA KURA ambazo hutolewa na Tume.

(ii) Tangazo la Uchaguzi la kituo lioneshe:

- (a) Tarehe ya upigaji kura;
- (b) Saa ya kufungua na kufunga vituo vya kupigia kura;
- (c) Sehemu ambapo waliojiandikisha kupiga kura watapiga kura zao; na
- (d) MFANO WA KARATASI ZA KURA ambazo hutolewa na Tume.

Wakati wa kutoa Tangazo la Uchaguzi ni vema yakabandikwa pia, Mabango ya Hadhari na Maelekezo kwa Wapiga Kura katika vituo vya kupigia kura na kwenye maeneo yenye watu wengi kwa mfano sokoni. Vile vile, Msimamizi wa Uchaguzi anatakiwa kubandika mabango mshale

kwenye barabara kuu na njia za kuingilia vituoni katika hali itakayowezesha wapiga kura kutambua vituo vya kupigia kura vilipo.

**Angalizo:**
Tangazo la Uchaguzi lisainiwe na Msimamizi wa Uchaguzi au Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi ngazi ya jimbo au kata. Mtu mwingine yeyote haruhusiwi.

### 9.4. Uteuzi wa Watendaji wa Vituo vya Kupigia Kura

Kwa mujibu wa kanuni ya 14 ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2020 na kanuni ya 12 ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020, Msimamizi wa Uchaguzi atateua Wasimamizi wa Vituo, Wasimamizi Wasaidizi wa Vituo vya Kupigia Kura na Makarani Waongozaji Wapiga Kura kwa idadi itakayoelekezwa na Tume ili kufanikisha upigaji kura.

#### (i) Sifa za Wasimamizi au Wasimamizi Wasaidizi wa Vituo vya Kupigia Kura

Ili mtu aweze kuteuliwa kuwa Msimamizi wa Kituo au Msimamizi Msaidizi wa Kituo anatakiwa awe na sifa zifuatazo:-

(a) Awe raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 au zaidi;

(b) Asiwe shabiki au kiongozi wa chama cha siasa;

(c) Awe mwadilifu, mtiifu na mwenye akili timamu;

(d) Awe amemaliza elimu ya kidato cha nne (4) au zaidi na anaweza kusoma na kuandika vizuri. Pia, anayeweza kuyaelewa Maelekezo ya Wasimamizi wa Vituo vya Kupigia Kura; na

(e) Ikiwezekana awe mkazi wa kata ambayo atafanyia kazi ya kusimamia upigaji kura na kuhesabu kura.

#### (ii) Sifa za Karani Mwongozaji Wapiga Kura

Ili mtu aweze kuteuliwa kuwa Karani Mwongozaji wa Wapiga Kura atapaswa kuwa na sifa zifuatazo: -

(a) Awe raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 au zaidi;

(b) Awe mkazi wa kata ambayo atafanyia kazi ya kuongoza wapiga kura;

(c) Ikiwezekana awe mpiga kura wa kituo anachofanyia kazi;

(d) Awe mwadilifu, mtiifu na mwenye akili timamu;

(e) Awe na elimu isiyopungua kidato cha nne na anayeweza kusoma na kuyaelewa Maelekezo kwa Makarani Waongozaji Wapiga Kura; na

(f) Asiwe shabiki au kiongozi wa chama cha siasa.

**9.5. Utaratibu wa Kuteua Watendaji wa Kituo**

Msimamizi wa Uchaguzi atafuata hatua zifuatazo ili kuwateua Msimamizi na Wasimamizi Wasaidizi wa Kituo na Karani Mwongozaji:-

(i) Kutangaza nafasi za kazi ili wenye sifa waweze kuomba;

(ii) Kupokea maombi;

(iii) Kuchambua sifa za waombaji;

(iv) Kuandaa orodha ya waombaji wenye sifa na kuibandika kwenye mbao za matangazo za kata na halmashauri;

(v) Kusaili walio na sifa; na

(vi) Kuteua na kuajiri kwa mkataba watendaji hao.

**Angalizo:**

Inasisitizwa kuwa watendaji watakaoteuliwa wawe na sifa zilizoainishwa katika maelekezo haya.

**9.6. Walinzi wa Vituo**

Msimamizi wa Uchaguzi awasiliane na Kamanda wa Polisi wa Wilaya ili kupata askari wa kulinda vituo vya kupigia kura.

**9.7. Mafunzo kwa Wasimamizi wa Vituo na Wasimamizi Wasaidizi wa Vituo na Makarani Waongozaji Wapiga Kura**

(i) Mafunzo kwa Wasimamizi au Wasimamizi Wasaidizi wa Vituo yafanyike kwa siku mbili (2) kwa utaratibu utakaowezesha kumalizika siku moja kabla ya siku ya uchaguzi. Mafunzo hayo yanaweza kufanyika kwa kata, kwa kadri Msimamizi wa Uchaguzi atakavyoona inafaa.

Mafunzo kwa Makarani Waongozaji Wapiga Kura yatafanyika kwa siku moja (1) kabla ya mafunzo ya Wasimamizi wa Vituo au Wasimamizi Wasaidizi wa Vituo.

(ii) Kabla ya kuanza kazi Wasimamizi wa Vituo, Wasimamizi Wasaidizi wa Vituo na Makarani Waongozaji Wapiga Kura wanatakiwa kuapa

kiapo cha kutunza siri na kutoa Tamko la kujitoa uanachama au kutokuwa mwanachama wa chama cha siasa.

## 9.8. Uteuzi na Wajibu wa Mawakala wa Upigaji Kura

### (i) Uteuzi wa Mawakala

Kwa mujibu wa kifungu cha 57 (1) na (2) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, na kifungu cha 58 (1) na (2) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, chama cha siasa kinaruhusiwa baada ya kupata ridhaa ya mgombea au wagombea kuteua na kuwasilisha kwa Msimamizi wa Uchaguzi orodha ya majina ya mawakala wa upigaji kura siku saba (7) kabla ya siku ya uchaguzi. Msimamizi wa Uchaguzi avitake vyama vya siasa kuwasilisha kwa maandishi majina ya Mawakala wa Upigaji kura, anuani na vituo walivyopangiwa kufanya kazi. Pia, vyama vya siasa viwasilishe barua za utambulisho wa kila wakala.

Kila chama cha siasa kitakuwa na wakala mmoja tu kwa kituo ambaye atawakilisha wagombea wa chama hicho kwa uchaguzi wa kiti cha Rais, Mbunge na Diwani katika kituo husika.

Kwa mujibu wa kanuni ya 50 (1) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2020 na kanuni ya 43 (1) ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020, Msimamizi wa Uchaguzi atapaswa kuvipatia vyama vya siasa orodha ya vituo vya kupigia kura siku kumi na nne (14) kabla ya Siku ya Uchaguzi.

### (ii) Utambulisho wa Mawakala wa Vyama vya Siasa

Kwa mujibu wa kanuni ya 50 (6) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2020 na kanuni ya 43 (6) ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020, barua ya utambulisho wa kila wakala itakayowasilishwa na chama iainishe kituo alichopangiwa na iambatishwe na picha mbili (*Passport size*) zilizopigwa si zaidi ya miezi mitatu.

Aidha, kwa mujibu wa kifungu 57 (3) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 chama kitaruhusiwa kuteua wakala mbadala endapo aliyeteuliwa awali amefariki au ameshindwa kutekeleza majukumu ya uwakala. Katika kurahisisha utekelezaji wa suala hili, sambamba na orodha ya mawakala wa vituoni, vyama viwasilishe majina mawili ya mawakala wa ziada kwa kila kata ambao watatumika kama mawakala mbadala iwapo itahitajika.

Endapo wakala hana picha anaweza kuwasilisha nakala mbili za mojawapo ya vitambulisho vifuatavyo: -

(a) Kadi ya mpiga kura;

(b) Kitambulisho cha Taifa;

(c) Leseni ya udereva; au

(d) Pasi ya kusafiria

Baada ya Msimamizi wa Uchaguzi kupokea utambulisho wa mawakala atafanya yafuatayo: -

(a) Ataandaa orodha ya mawakala kwa kila kituo.

(b) Ataikabidhi orodha hiyo kwa Wasimamizi wa vituo pamoja na barua ya utambulisho yenye picha wakati wa kugawa vifaa. Kama barua haina picha iambatishwe na nakala moja ya vitambulisho vilivyotajwa hapo juu.

(c) Atawaelekeza Wasimamizi wa Vituo kubandika orodha ya mawakala watakayopatiwa nje ya kituo cha kupigia kura kabla ya kuanza kwa zoezi la upigaji kura.

(d) Atawaelekeza Wasimamizi wa Vituo wasiombe utambulisho mwingine wowote kutoka kwa mawakala wa vyama.

**(iii) Kiapo cha Kutunza Siri**

Kwa mujibu wa kanuni ya 50 (4) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2020 na kanuni ya 43 (4) ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020, mawakala wa upigaji kura wanatakiwa kuapa kiapo cha kutunza siri mbele ya Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi siku saba (7) kabla ya Siku ya Uchaguzi kwa kutumia Fomu Na. 6. Wakala ambaye hajaapa kiapo cha kutunza siri hataruhusiwa kuingia kwenye kituo cha kupigia kura.

Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 93 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 92 cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, endapo Mgombea atahitaji kuingia kwenye vituo vya kupigia, kuhesabia au kujumlishia kura, atatakiwa kabla ya kufanya hivyo kuapa kiapo cha kutunza siri mbele ya Msimamizi wa Uchaguzi kwa mujibu wa sheria.

**(iv) Wajibu wa Mawakala**

Wajibu wa mawakala wa upigaji kura ni:-

(a) Kumtambua mpiga kura anayetaka kupiga kura kuwa ndiye mwenye jina lililoandikwa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura;

(b) Kumwakilisha na kulinda maslahi ya mgombea au wagombea kituoni;

(c) Kushirikiana na Msimamizi wa Kituo na Msimamizi Msaidizi wa Kituo katika kuhakikisha kwamba mwenendo wa upigaji kura kituoni unazingatia masharti ya Sheria na taratibu zilizowekwa;

(d) Kujaza Fomu Na. 14 na Na. 16 kituoni, kwa mujibu wa Sheria za Uchaguzi; na

(e) Kukiwakilisha chama chake kwenye zoezi la kuhesabu kura baada ya kukamilika kwa zoezi la upigaji kura kwani wakala wa upigaji ndiye atakuwa wakala wa kuhesabu kura.

Ili waweze kutekeleza kazi hizo kwa ufanisi, Tume inashauri kwamba:-

(a) Vyama vya siasa viteue mawakala wa upigaji kura wanaowaamini ikiwezekana kutoka miongoni mwa watu waliojiandikisha kuwa wapiga kura kwenye maeneo yenye vituo ambavyo watafanyia kazi.

(b) Viongozi wa vyama vya siasa wanawajibika kuwafundisha mawakala wao taratibu zote za kupiga na kuhesabu kura kituoni.

Aidha, Tume imeandaa vijitabu vya Maelekezo kwa Mawakala wa vyama vya siasa. Wasimamizi wa Uchaguzi wanatakiwa kuvipatia vyama vya siasa vinavyoshiriki uchaguzi vijitabu hivyo kwa idadi ya mawakala wao.

**Angalizo:**

1. Nakala ya fomu ya kiapo (Fomu Na. 6) haitatumika kwa ajili ya utambulisho wa wakala na wakala hatapewa nakala ya fomu hizo baada ya kuapa.
2. Vilevile, gharama za mawakala wa vyama vya siasa zitalipwa na vyama vyao.

### 9.9. Fomu na Vifaa vya Upigaji Kura

Fomu na vifaa vitakavyotumika siku ya uchaguzi vitatakiwa kugawanywa kwa kuzingatia mahitaji halisi ya vituo. Msimamizi wa Uchaguzi anatakiwa kuhakikisha zoezi la upangaji wa vifaa vya vituo linakamilika kabla ya mafunzo ya watendaji wa vituo ili baada ya mafunzo avigawe kwa Wasimamizi wa Vituo. Fomu na vifaa hivyo ni kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 1:-

**Jedwali Na. 1: Orodha ya Fomu na Vifaa vinavyotumika siku ya Uchaguzi Kituoni**

| Na. | Aina ya Kifaa | Matumizi |
|---|---|---|
| 1. | Sanduku la Kura.<br>Sanduku la kila uchaguzi litakuwa na mfuniko wenye rangi tofauti kama ifuatavyo:<br>- Bluu kwa uchaguzi wa kiti cha Rais<br>- Nyeusi kwa uchaguzi wa Wabunge<br>- Nyeupe kwa uchaguzi wa Madiwani. | Hutumika kutumbukiza karatasi za kura baada ya mpiga kura kupiga kura yake. |
| 2. | Karatasi za kura. | Hutumika kwa ajili ya wapiga kura kupiga kura kwa uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani. |
| 3. | Muhuri wa Kituo. | Hutumika kugonga Karatasi ya Kura kabla mpiga kura hajakabidhiwa kwenda kwenye kituturi. Pia hutumika kugonga vibali vya watendaji au mawakala (Fomu Na. 18) na vibali vya wagombea (Fomu Na. 19) na Fomu nyingine kama itakavyoelekezwa na Tume. |
| 4. | Kibweta/kidau cha Wino (*stamp pad*). | Hutumika kwa ajili ya muhuri wa kituo. |
| 5. | Wino wa Kidau (*stamp pad ink*). | Huwekwa kwenye kibweta au kidau. |
| 6. | Wino maalum usiofutika (*indelible ink).* | Hupakwa katika kidole cha mwisho cha mkono wa kushoto baada ya mpiga kura kukamilisha upigaji kura kabla ya kutoka kituoni. |
| 7. | Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. | Hutumika kuthibitisha wapiga kura wanaostahili kupiga kura katika kituo husika. |

| Na. | Aina ya Kifaa | Matumizi |
|---|---|---|
| 8. | Orodha ya Majina ya Wapiga Kura (Nakala 2). | Hubandikwa nje ya kituo kuonesha majina ya wapiga kura wa kituo hicho. Nakala moja hutumiwa na Karani Mwongozaji Wapiga Kura kwa kuwasaidia wapiga kura kufahamu mahali walipopangiwa kupiga kura zao. |
| 9. | Fomu Na. 13 – Hesabu ya karatasi za kura. | Ni fomu ya kujaza idadi ya karatasi za kura zilizopokelewa na namba zake ambazo hujazwa kabla ya kuanza upigaji kura. Vilevile, hutumika kujaza idadi ya karatasi za kura zilizotumika, zilizoharibika na zisizotumika baada ya kukamilika upigaji kura kituoni. |
| 10. | Fomu Na. 14<br>Kuridhika au kutoridhika kwa wakala wa upigaji kura kabla ya kuanza upigaji kura na baada ya upigaji kura. | Hujazwa na mawakala wa upigaji kura kabla ya kuanza upigaji kura na baada ya kukamilika upigaji kura kuonesha kuridhika au kutoridhika na maandalizi na mwenendo wa upigaji kura kituoni. |
| 11. | Fomu Na. 15<br>Malalamiko ya mpiga kura kuhusu mwenendo wa Upigaji Kura katika Kituo. | Hujazwa na mpiga kura ambaye ana malalamiko juu ya mwenendo wa upigaji kura au utendaji kazi wa Msimamizi wa Kituo au Msimamizi Msaidizi wa Kituo. |
| 12. | Fomu Na. 16<br>Kuridhika au kutoridhika kwa Mgombea au Wakala katika Hatua ya Kuhesabu Kura. | Hujazwa na wakala au mgombea katika hatua za kuhesabu kura kuonesha kuridhika au kutoridhika na mwenendo wa kuhesabu kura kwa mujibu wa sheria. |
| 13. | Fomu Na. 17 – Tamko la Mpiga Kura. | Tamko hili hutolewa na mpiga kura aliyetiliwa shaka na Msimamizi wa Kituo au Wakala kuwa amekwisha piga kura au hana haki ya kupiga kura. |

| Na. | Aina ya Kifaa | Matumizi |
|---|---|---|
| 14. | Fomu Na. 18 – Kibali cha kumwezesha Mtendaji wa Uchaguzi au Wakala wa chama cha siasa kupiga kura kituo ambacho hakujiandikisha. | Hutumika kuwaruhusu watendaji wa uchaguzi walioainishwa kwa mujibu wa sheria na mawakala wa vyama vya siasa kupiga kura katika vituo ambavyo hawakujiandikisha katika jimbo au kata husika. |
| 15. | Fomu Na. 19 – Kibali cha kumwezesha Mgombea Kupiga Kura kwenye Kituo ambacho hakujiandikisha. | Hutumika kuwaruhusu wagombea wa nafasi mbalimbali kupiga kura katika vituo ambavyo hawakujiandikisha katika jimbo au kata husika. |
| 16. | Fomu Na. 20 – Taarifa ya Msimamizi wa Kituo cha Kupigia Kura. | Hutumiwa na Msimamizi wa Kituo kujaza taarifa mbalimbali za kituo baada ya kufunga kituo. |
| 17. | Bahasha ya Kituo. | Hutumika kuhifadhi vifaa mbalimbali vinavyohusika katika kituo cha kupigia kura. |
| 18. | Seti ya lakiri za plastiki za kufungia masanduku (*seals*) | Hutumika kufungia masanduku ya kura kabla ya kuanza upigaji kura, wakati wa kufunga kituo na baada ya kumaliza zoezi la kuhesabu kura. |
| 19. | Utepe wa gundi (*cellotape*) | Hutumika kubandika matangazo yanayohusiana na uchaguzi kituoni. |
| 20. | Gundi ya Maji. | Hutumika kubandika matangazo yanayohusiana na uchaguzi kituoni. |
| 21. | Pini za kubandikia matangazo (*drawing pins*). | Hutumika kubandikia matangazo yanayohusiana na uchaguzi kituoni. |
| 22. | Karatasi maalum ya kukaushia wino (*blotting papers*). | Hutumika kufyonza wino unaomwagika. |
| 23. | Wembe. | Hutumika kukata tepe za kufungia masanduku. |
| 24. | Bahasha Namba, 2A, 2B, 2C, 3A, 3B, 3C, 4, 5A, 5B, 5C, 6A, 6B, 6C, 7A, 7B, 7C, 8A, 8B, 8C na 9. | Hutumika kuhifadhi nyaraka mbalimbali kama zilivyofafanuliwa katika kijitabu cha Maelekezo kwa |

| Na. | Aina ya Kifaa | Matumizi |
|---|---|---|
| | | Wasimamizi wa Vituo vya Kupigia Kura. |
| 25. | Karatasi za kuandikia (*writing pads)*. | Hutumika kuweka kumbukumbu ya taarifa mbalimbali zinazohusiana na masuala ya uchaguzi kituoni. |
| 26. | Kalamu za wino. | Hutumika kuandikia na kuweka alama ya vema (√) katika karatasi ya kura na kujaza fomu mbalimbali za kituoni. |
| 27. | Bango – Kituo cha Kupigia Kura. | Hutumika kutambulisha kituo cha kupigia kura. |
| 28. | Bango – Mshale. | Hutumika kuelekeza kituo cha kupigia kura kilipo. Mabango hayo yanapaswa kubandikwa barabarani na kwenye njia za kuelekea mahali kilipo kituo chaa kupigia kura. |
| 29. | Bango – Hadhari na Maelekezo kwa Wapiga Kura. | Hutumika kueleza mambo ya kujihadhari kuhusiana na mchakato wa uchaguzi na taratibu za upigaji kura. |
| 30. | Mfano wa karatasi ya kura kwa Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani. | Huonesha namna karatasi ya kura itakavyokuwa. Huonesha jina, picha, vifupisho vya majina na nembo za vyama husika pamoja na sehemu ya kuweka alama. |
| 31. | Taa na betri zake. | Hutumika kwa ajili ya kutoa mwanga pale ambapo kutakuwa na giza kwenye kituo cha kupigia kura na kuhesabia kura. |
| 32. | Jalada la Nukta Nundu (*tactile ballot folder*) kwa ajili ya wasioona. | Ni kifaa kinachotumika kuwawezesha wapiga kura wasioona kupiga kura wenyewe kwa kutumia alama za nukta nundu . |
| 33. | Vituturi (*polling booths*). | Hutumika kuwawezesha wapiga |

| Na. | Aina ya Kifaa | Matumizi |
|---|---|---|
| | | kura kupiga kura kwa siri kwa mujibu wa sheria. Kwa wale wenye ulemavu wa miguu kituturi kigeuzwe chini-juu (*upside-down*) ili kiwe kifupi. Hii itawawezesha kupiga kura kwa urahisi. |
| 34. | Vitabu vya Fomu za Matokeo ya uchaguzi: 21A, 21B, 21C SEHEMU A na SEHEMU B. | SEHEMU A ya fomu husika hutumika kujaza matokeo ya kila mgombea kituoni.<br>SEHEMU B ya fomu husika hutumika kujaza kura zenye mgogoro. |
| 35. | *Rubber bands* | Hutumika kufunga bahasha na karatasi mbalimbali zinazotumika kituoni. Hutumika pia, wakati wa kuhesabu kura kufunga karatasi za kura kabla ya kuziweka kwenye bahasha husika. |

Msimamizi wa Uchaguzi atawajibika kupanga utaratibu mzuri wa usafiri wa watendaji na vifaa wakati wa kwenda vituoni na kuvipeleka mahali pa kujumlishia kura.

### 9.10. Makabidhiano na Usalama wa Vifaa vya Kupigia Kura

(i) Wasimamizi wa Vituo watakabidhiwa kwa maandishi vifaa vyote vinavyotumika katika kituo cha kupigia kura, siku moja kabla ya Siku ya Upigaji Kura.

(ii) Makabidhiano ya vifaa kati ya Msimamizi wa Uchaguzi na Wasimamizi wa Vituo yashuhudiwe na wagombea au wawakilishi wao. Msimamizi wa Uchaguzi anawajibu wa kuwataarifu wagombea kuhusu mahali na muda ambao vifaa vitagawanywa.

(iii) Wagombea wapatiwe orodha kamili ya vifaa muhimu vitakavyotolewa kwa kila kituo.

(iv) IIi kurahisisha zoezi hili, Msimamizi wa Uchaguzi atatakiwa kuandaa mapema orodha inayoonesha kituo, idadi ya wapiga kura, namba za masanduku ya kupigia kura yaliyopangwa, idadi na

namba za karatasi za kura zilizotolewa kwa kituo hicho na lakiri za plastiki kwa kila sanduku la kupigia kura.

(v) Mawakala watahakikisha kwamba masanduku ya kupigia kura na vifaa vingine viko salama na kwamba hakuna udanganyifu au hila zinazofanyika.

(vi) IIi utekelezaji wa suala hili uwe na mafanikio, ni muhimu Wasimamizi wa Uchaguzi wawapatie wagombea utaratibu wa misafara ya magari. Ni muhimu kukumbuka kuwa, kutakuwa na msafara wa kwanza wa kubeba masanduku na fomu za matokeo ya uchaguzi wa Rais na Wabunge na msafara wa pili wa kubeba masanduku na fomu za matokeo ya uchaguzi wa Madiwani.

(vii) Wagombea waelezwe kwamba mawakala wa upigaji kura watakaosimamia vituo vya mbali ambako misafara ya kukusanya masanduku na vifaa vingine itaanzia, ndio watakaosindikiza na watakaoshuhudia makabidhiano ya vifaa katika kituo cha kujumlishia kura.

(viii) Mbali na hatua zilizochukuliwa na Tume, wagombea watakuwa huru kusindikiza misafara ya magari yenye masanduku ya kura kwa utaratibu utakaokubaliwa na Msimamizi wa Uchaguzi na kwa gharama zao wenyewe. Usalama wa misafara rasmi, kama ilivyopangwa na Msimamizi wa Uchaguzi uwe moja wapo ya vigezo vikubwa vya kumsaidia Msimamizi wa Uchaguzi kuruhusu au kutoruhusu usindikizaji nje ya utaratibu rasmi unaogharamiwa na Tume.

### 9.11. Vibali vya Watendaji wa Uchaguzi, Mawakala na Wagombea Kupiga Kura Vituo Ambavyo Hawakujiandikisha Fomu Na. 18 na Na. 19

Watendaji na mawakala ambao kutokana na majukumu yao katika uchaguzi hawataweza kupiga kura katika vituo walivyojiandikisha watapatiwa vibali maalum kwa kujaziwa Fomu Na. 18 na Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata ili waruhusiwe kupiga kura katika vituo watakapofanyia kazi.

Endapo mtendaji au wakala anayehusika atapangiwa kufanya kazi nje ya kata aliyojiandikisha hatapiga kura ya Diwani. Kwa halmashauri zenye jimbo zaidi ya moja, mtendaji au wakala atakayepangiwa nje ya jimbo alipojiandikisha hatapiga kura ya Mbunge wala Diwani bali atapiga kura ya Rais tu.

Wagombea ambao watahitaji kupiga kura katika vituo ambavyo hawakujiandikisha watapatiwa vibali maalum kwa kujaziwa Fomu Na. 19 na Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata ambavyo vitawawezesha kupiga Kura katika kituo chochote katika jimbo au kata yake. Aidha, mgombea Ubunge hataruhusiwa kupiga kura katika jimbo ambalo hakujiandikisha, vivyo hivyo kwa mgombea wa nafasi ya Udiwani katika kata.

Kabla mpiga kura aliyetumia Fomu Na. 18 au Fomu Na. 19 hajaondoka, Msimamizi wa Kituo achukue fomu ya mpiga kura huyo aigonge muhuri wa kituo na kuweka katika bahasha Na. 4.

**Angalizo:**

Ni vema watendaji, mawakala na wagombea watakaopiga kura nje ya vituo walivyojiandikisha wakajulikana mapema ili vibali hivyo viandaliwe na kugawiwa kwa wahusika kabla ya Siku ya Uchaguzi.

### 9.12. Kuahirisha Upigaji Kura

Iwapo kabla ya upigaji kura au Siku ya Kupiga Kura yatatokea matukio yatakayozuia upigaji kura kufanyika kama ilivyopangwa katika jimbo au kata, Msimamizi wa Uchaguzi ataijulisha haraka Tume ili ipange tarehe nyingine ya uchaguzi kwa ajili ya jimbo au kata husika.

### 9.13. Siku ya Kupiga Kura

(i) Siku ya kupiga kura inapangwa na Tume kwa mujibu wa kifungu cha 46 (1) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, na kifungu cha 48 (1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292. Siku ya Uchaguzi itakuwa si chini ya siku sitini (60) na si zaidi ya siku tisini (90) baada ya uteuzi wa wagombea kufanyika.

(ii) Aidha, kwa chaguzi ndogo kwa mujibu wa kifungu cha 46 (2) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, na kifungu cha 48 (2) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, Siku ya Uchaguzi itakuwa si zaidi ya siku thelathini (30), baada ya uteuzi wa wagombea kufanyika.

### 9.14. Namna ya Kuendesha Zoezi la Upigaji Kura

(i) Zoezi la upigaji kura litafanyika kama ifuatavyo: -

(ii) Kituo cha kupigia kura kitafunguliwa saa moja kamili (1:00) asubuhi. Msimamizi wa Kituo cha Kupigia Kura atatakiwa kuwasili katika kituo chake kabla ya muda huo;

(iii) Msimamizi wa Kituo anatakiwa akague mazingira ya kituo chake kuhakikisha kuwa hakuna matangazo ya kampeni ya mgombea yeyote. Baada ya hapo atabandika bango la kituo cha kupigia kura, bango mshale, bango la hadhari na maelekezo kwa mpiga kura na mfano wa Karatasi ya Kura;

(iv) Msimamizi wa Kituo aandae mpangilio wa kituo ikiwa ni pamoja na eneo watakalokaa watendaji, mawakala, watazamaji, sanduku la kura na eneo la kuweka kitututi kwa ajili ya kupigia kura;

(v) Msimamizi wa Kituo atawaonesha mawakala wa upigaji kura na mtu yeyote atakayekuwepo katika kituo cha kupiga kura kwamba sanduku la kura ni tupu, ili waweze kuhakikisha kuwa halina kitu chochote ndani yake;

(vi) Kabla ya upigaji kura kuanza, Msimamizi wa Kituo atawapa mawakala (kama wapo) Fomu Na. 14 wajaze ili kutoa maoni kama wanaridhika au hawaridhiki na matayarisho ya kituo cha kupigia kura;

(vii) Muda wa kufungua kituo ukifika, Msimamizi wa Kituo afungue kituo na kuwaruhusu wapiga kura kuanza kupiga kura hata kama mawakala hawajafika. Wanaoruhusiwa kupiga kura ni wale ambao wameandikishwa kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura; na

(viii) Mpiga kura aliyejiandikisha lakini amepoteza sifa za kuwa mpiga kura haruhusiwi kupiga kura.

**9.15. Matumizi ya Fomu Na. 17**

Fomu hii hujazwa iwapo Msimamizi wa Kituo, wakala au mgombea atatilia shaka utambulisho wa mpiga kura yeyote anayetaka kupiga kura kuwa hana haki ya kupiga kura au tayari amepiga kura. Msimamizi wa Kituo atampa tahadhari mpiga kura huyo kwamba ni kosa kwa mtu kupiga kura kama hana haki kwa mujibu wa sheria na kwamba, anaweza kushtakiwa mahakamani. Mpiga kura huyo akizidi kudai kupiga kura, Msimamizi wa Kituo atamtaka kutoa Tamko katika Fomu Na. 17 na kisha amruhusu kupiga Kura. Mpiga kura akikataa kutoa tamko asiruhusiwe kupiga kura.

Mpiga kura huyo ni sharti awe na Kadi ya Mpiga Kura na awemo kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura la kituo husika. Fomu Na. 17 siyo mbadala wa kadi ya mpiga kura.

**9.16. Wanaoruhusiwa Kuingia Kwenye Kituo cha Kupigia Kura**

Kwa mujibu wa kifungu cha 63 (2) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 63 (2) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 wafuatao ndio wanaoruhusiwa kuingia kwenye kituo cha kupigia kura:-

(i) Msimamizi wa Kituo;

(ii) Msimamizi Msaidizi wa Kituo;

(iii) Mawakala wa Upigaji Kura;

(iv) Wapiga Kura kwa ajili ya kupiga kura tu;

(v) Mtu anayemsaidia mpiga kura asiyeweza kupiga kura mwenyewe kwa sababu ya ulemavu au asiyejua kusoma;

(vi) Mtazamaji wa Uchaguzi aliyeidhinishwa na mwenye kitambulisho maalum kilichotolewa na Tume;

(vii) Mgombea;

(viii) Mjumbe wa Tume;

(ix) Mkurugenzi wa Uchaguzi;

(x) Afisa wa Tume;

(xi) Askari polisi au mtu anayehusika na usalama wa kituo cha kupigia kura;

(xii) Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi; na

Mratibu wa Uchaguzi wa Mkoa.

| |
|---|
| **Angalizo:** Watazamaji wa Uchaguzi watapewa vitambulisho maalum kutoka Tume ambavyo vitatumika kuwatambulisha vituoni. |

**9.17. Utaratibu wa Kufunga Kituo**

Kwa mujibu wa kifungu cha 68 na 69 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 69 na 70 cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 kituo cha kupigia kura kitafungwa saa kumi kamili (10:00) jioni.

(i) Endapo kutakuwa na wapiga kura kwenye mstari muda huo, mlinzi wa kituo atasimama nyuma ya mpiga kura wa mwisho ili mpiga kura mwingine yeyote aliyechelewa asiweze kuja na kupanga foleni mara baada ya muda wa kufunga kituo kufika. Wapiga kura walio kwenye mstari waruhusiwe kupiga kura hadi watakapokamilisha upigaji kura.

(ii) Wapiga kura watakaofika kwenye kituo cha kupigia kura baada ya saa kumi kamili (10:00) jioni watakuwa wamechelewa na hawataruhusiwa kupiga kura.

(iii) Mara baada ya mtu wa mwisho kupiga kura Msimamizi wa Kituo atawapa mawakala Fomu Na. 14 ili wajaze kuonesha kama wanaridhika au hawaridhiki na mwenendo wa Upigaji Kura.

(iv) Msimamizi wa Kituo anatakiwa ayafunge masanduku ya kura na ajaze Fomu Na. 13 kuonesha matumizi ya karatasi za kura.

**9.18. Kuhesabu Kura**

Kwa mujibu wa kifungu cha 70A cha Sheria Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 70A cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, kura zitahesabiwa katika vituo vya kupigia kura. Mara baada ya kufunga kituo cha kupigia kura, kituo hicho kitageuka kuwa kituo cha kuhesabia kura.

Endapo kutakuwa na sababu za kiusalama au sababu nyingine za msingi Msimamizi wa Kituo baada ya kushauriana na mawakala au kwa kushauriwa na Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi au Mawakala, anaweza kuamua kura zihesabiwe katika kituo kingine cha kupigia kura au sehemu nyingine. Katika kuhesabu kura itahakikishwa kwamba kura zitakazohesabiwa hazitachanganywa na hesabu ya kura za vituo vingine.

Wanaoruhusiwa kuingia katika kituo cha kuhesabia kura ni:-

(a) Msimamizi wa Kituo;

(b) Msimamizi Msaidizi wa Kituo;

(c) Mgombea kama atakuwepo;

(d) Wakala wa Upigaji Kura;

(e) Mtazamaji wa Uchaguzi aliyeidhinishwa na mwenye kitambulisho maalum kilichotolewa na Tume;

(f) Mjumbe wa Tume ya Uchaguzi;

(g) Mkurugenzi wa Uchaguzi;

(h) Afisa wa Tume;

(i) Mratibu wa Uchaguzi wa Mkoa;

(j) Msimamizi wa Uchaguzi;

(k) Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi; na

(l) Askari polisi au mtu anayehusika na usalama wa mahali pa kuhesabia kura.

**Angalizo:**

1. Watazamaji wa Uchaguzi watapewa vitambulisho maalum kutoka Tume ambavyo vitatumika kuwatambulisha vituoni.
2. Msimamizi wa Kituo ahakikishe kuwa mtu yeyote asiyehusika hatakiwi kuwepo eneo la kuhesabia kura.

### 9.18.1 Alama Zinazokubalika Katika Karatasi ya Kura

Alama inayokubalika katika kupiga kura ni alama ya vema (√) lakini iwapo mpiga kura atashindwa kuweka alama hii kama inavyotakiwa, alama yoyote inayoonesha wazi kwamba mpiga kura alitarajia kumchagua nani ikubaliwe.

Alama hizo ni pamoja na 'X', ili mradi tu iwe katika chumba kilichopo wazi. Kama mpiga kura atashindwa kuweka alama katika chumba kilichopo wazi na badala yake akaweka alama hiyo kwenye jina la mgombea au chama chake, alama hiyo inakubalika na ni kura iliyo halali.

### 9.18.2 Uamuzi wa Kuwa Kura ni Halali au Siyo Halali

Wakati wa kuhesabu kura uamuzi wa mwisho kuhusu uhalali wa kura itakayohesabiwa ni wa Msimamizi wa Kituo. Hivyo, endapo Msimamizi wa Kituo ataridhika kuwa kura imeharibika au batili ataikataa na haitahesabiwa na ataandika nyuma ya kura "IMEKATALIWA". Endapo uamuzi huo utapingwa Msimamizi wa Kituo ataandika nyuma ya kura "UAMUZI UMEPINGWA NA………..’’ (ataandika jina la wakala na chama cha aliyepinga). Kisha ataweka kura katika Bahasha Na.5 (A, B au C) na kuwasilishwa kwa Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi kwa ajili ya uamuzi.

Msimamizi wa Kituo cha kupigia kura atajaza fomu ya matokeo ya uchaguzi katika kituo kwa kila uchaguzi yaani 21A (uchaguzi wa Rais),

21B (uchaguzi wa Bunge) na 21C (uchaguzi wa Madiwani) SEHEMU B ambapo ataonesha matokeo ya wagombea kama yalivyothibitishwa kituoni.

#### 9.18.3 Kura Zilizoharibika

Karatasi ya Kura haitahesabiwa kuwa kura halali iwapo kura hiyo:-

(i) Haina muhuri wa kituo,

(ii) Imepigwa kwa mgombea zaidi ya mmoja,

(iii) Ina alama, au maandishi yanayoweza kumtambulisha mtu aliyepiga Kura,

(iv) Haina alama yoyote, na

(v) Amepigiwa mgombea aliyejitoa.

Kila mgombea au wakala atatakiwa kujaza Fomu Na. 16 kuonesha kuridhika au kutoridhika kwake baada ya kukagua masanduku ya kura, kuthibitisha idadi ya karatasi za kura zilizomo katika kila sanduku na kuhesabu kura alizopata kila mgombea.

**Angalizo:**

Wakati wa kuhesabu kura, kura za wagombea zitakazokutwa katika sanduku lisilohusika **zisichukuliwe** kuwa ni kura zilizokataliwa. Kura hizo zitahamishiwa katika sanduku linalohusika na kuhesabiwa pamoja na kura zingine. Kwa mfano, kura za uchaguzi wa Rais zitakazokutwa kwenye sanduku la kura za Mbunge au Diwani zitahesabiwa pamoja na kura za Rais. Zoezi la kuhesabu kura likishaanza ni lazima liendelee mfululizo hadi litakapokamilika.

### 9.19. Ujazaji wa Fomu ya Matokeo ya Uchaguzi Kituoni

Fomu za matokeo ya uchaguzi kituoni Na. 21A, 21B na 21C zimegawanyika sehemu mbili: **SEHEMU A na SEHEMU B.** Kila sehemu itakuwa katika **kitabu chake.** Kila kitabu kitakuwa na kurasa **ishirini** na nne (24) ambazo zimetenganishwa na karatasi ngumu (*separator*). Karatasi zake zimetayarishwa katika namna ambayo inawezekana kuandika na kutoa nakala bila kuweka karatasi ya kaboni (*Carbon papers*) yaani ni "*Self copying*".

**Kitabu cha matokeo ya uchaguzi Kituo Na. 21A, 21B, 21C SEHEMU A**: Sehemu hii itajazwa matokeo ya kura alizopata kila mgombea baada ya hatua ya kuhesabu kura kukamilika. Vilevile, itaonesha idadi ya wapiga kura walioandikishwa, waliopiga kura, kura halali, kura zenye mgogoro na kura zilizokataliwa. Kitabu kitakuwa na kurasa 24 ambazo mgawanyo wake utakuwa kama inavyoonesha kwenye *Jedwali Na. 2*:

**Jedwali Na. 2: Mgawanyo wa kurasa za kitabu cha Fomu Na. 21A, 21B, na 21C Sehemu A**

| Kurasa | Chapa (*label*) za Kurasa | Matumizi |
|---|---|---|
| Ukurasa Na. 1 | **Nyaraka Halisi (*original*)** | **Msimamizi wa Uchaguzi** |
| **Ukurasa Na. 2** | **Nakala ya kwanza** | **Kubandika nje ya kituo cha kupigia kura** |
| Ukurasa Na. 3 | Nakala ya pili | Wakala |
| Ukurasa Na. 4 | Nakala ya tatu | Wakala |
| Ukurasa Na. 5 | Nakala ya nne | Wakala |
| Ukurasa Na. 6 | Nakala ya tano | Wakala |
| Ukurasa Na. 7 | Nakala ya sita | Wakala |
| Ukurasa Na. 8 | Nakala ya saba | Wakala |
| Ukurasa Na. 9 | Nakala ya nane | Wakala |
| Ukurasa Na. 10 | Nakala ya tisa | Wakala |
| Ukurasa Na. 11 | Nakala ya kumi | Wakala |
| Ukurasa Na. 12 | Nakala ya kumi na moja | Wakala |
| **Karatasi ngumu (*separator*)** | | |
| Ukurasa Na. 13 | **Nyaraka Halisi** | **Kwa matumizi ya Tume** |
| Ukurasa Na. 14 | Nakala ya kumi na mbili | Wakala |
| Ukurasa Na. 15 | Nakala ya kumi na tatu | Wakala |
| Ukurasa Na. 16 | Nakala ya kumi na nne | Wakala |
| Ukurasa Na. 17 | Nakala ya kumi na tano | Wakala |
| Ukurasa Na. 18 | Nakala ya kumi na sita | Wakala |
| Ukurasa Na. 19 | Nakala ya kumi na saba | Wakala |
| Ukurasa Na. 20 | Nakala ya kumi na nane | Wakala |
| Ukurasa Na. 21 | Nakala ya kumi na tisa | Wakala |
| Ukurasa Na. 22 | Nakala ya ishirini | Wakala |
| Ukurasa Na. 23 | Nakala ya ishirini na moja | Wakala |
| Ukurasa Na. 24 | Nakala ya ishirini na mbili | Wakala |

Karatasi ya mwanzo (Uk. Na. 1) yaani nyaraka halisi (*Original*) itatumiwa na Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi wakati wa kujumlisha matokeo ya uchaguzi.

Ujazaji wa karatasi hizo utategemea idadi ya mawakala waliopo kituoni. Karatasi ya kumi na tatu (13) itajazwa tu iwapo vyama vitakavyoshiriki katika uchaguzi ni zaidi ya kumi (10) kwa kuwa kila wakala anaweza kupatiwa nakala ya matokeo ya uchaguzi ya kituo.

**Kitabu cha Matokeo ya Uchaguzi ya Kituo Na. 21A, 21B na 21C SEHEMU B:** Mpangilio wa kitabu hiki utafanana na mpangilio wa kitabu cha matokeo ya uchaguzi ya Kituo **SEHEMU A**. Fomu hizo za **SEHEMU B** zitajazwa iwapo kutajitokeza **Kura zenye mgogoro** katika kituo na Msimamizi wa Kituo ameshindwa kuziamulia na kuhitaji kuzipeleka kwa Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ili kufanya uamuzi.

Hivyo, Msimamizi wa Kituo atapaswa kujaza fomu za matokeo ambazo ni fomu **Na. 21A, 21B na 21C SEHEMU B**, upande ulioandikwa "SEHEMU HII IJAZWE KABLA YA KUSHUGHULIKIA KURA ZENYE MGOGORO" kama alivyojaza katika kitabu cha matokeo **SEHEMU A** na kukiweka kitabu hicho katika Bahasha Na. 8A, 8B na 8C kisha kukabidhi kwa Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi.

Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atatoa uamuzi wa kura hizo na kukamilisha Fomu husika ambayo ilijazwa kituoni na kuachwa sehemu ya maamuzi ya kura zenye mgogoro. Baada ya kutoa uamuzi mawakala au wagombea waliopo watasaini na Msimamizi wa Uchaguzi anaweza kuwapatia nakala.

Kama ilivyo katika **SEHEMU A** ya Fomu ya Matokeo ya uchaguzi ya Kituo, Karatasi iliyoandikwa KWA MATUMIZI YA TUME itakabidhiwa kwa Afisa anayeingiza matokeo ya kura katika Mfumo wa Matokeo ya uchaguzi ili aweze kuingiza uamuzi wa kura zenye **Mgogoro** na **zilizoharibika.**

Fomu zote zilizoandikwa KWA MATUMIZI YA TUME zitatakiwa kupelekwa Makao Makuu ya Tume kwa ajili ya uhakiki wa matokeo baadaye.

Katika kujaza fomu za matokeo ya uchaguzi kituoni, Msimamizi wa Kituo akumbuke: -

(i) Kuweka alama ya vema **(**√**)** kwa mgombea aliyepata kura nyingi zaidi;

(ii) Kuandika jina lake, kusaini na kuwapa mawakala au wagombea waandike majina yao na kusaini;

(iii) Kubandika nakala moja ya matokeo ya Uchaguzi wa Rais, Ubunge na Madiwani sehemu ya wazi nje ya kituo cha kupigia kura. Nakala

itakayobandikwa ni **nakala ya pili kutoka katika kitabu cha matokeo husika;**

(iv) Kumpa kila wakala nakala moja ya matokeo ya uchaguzi kwa kila uchaguzi katika kituo chake;

(v) Kujaza Fomu Na. 20 kwa ukamilifu; na

(vi) Kupeleka masanduku ya kura, vifaa na fomu za matokeo ya uchaguzi ya sehemu ya kujumlishia kura:

(a) Kwa uchaguzi wa Rais na Wabunge, Msimamizi wa Kituo cha Kupigia Kura, Mlinzi wa Kituo na Mawakala watapeleka masanduku ya kura, fomu za matokeo ya uchaguzi na vifaa vyote vinavyohusika kwa Msimamizi wa Uchaguzi.

(b) Kwa uchaguzi wa Madiwani, Msimamizi Msaidizi wa Kituo cha Kupigia Kura, Mlinzi wa Kituo na Mawakala watapeleka masanduku ya kura, fomu za matokeo ya uchaguzi na vifaa vyote vinavyohusika na uchaguzi wa Madiwani kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi.

(c) Ni muhimu kuweka utaratibu mzuri wa namna ambavyo misafara yote ya aina mbili itakuwa na walinzi pamoja na mawakala. Msafara kwa ajili ya fomu za matokeo ya uchaguzi na masanduku ya uchaguzi wa Rais na Wabunge uende moja kwa moja sehemu ya kujumlishia kura za uchaguzi wa Rais na Wabunge. Hii itasaidia matokeo kujumlishwa na kutangazwa mapema.

**Angalizo:** Fomu za Matokeo ya uchaguzi zilizoandikwa KWA MATUMIZI YA TUME kutoka katika kitabu cha Matokeo ya uchaguzi ya Kituo na **SEHEMU B** ya fomu hizo iliyojazwa kura zenye Mgogoro ikiwa katika kitabu chake zitawekwa kwenye Bahasha Na. 8A, 8B na 8C.

Fomu za matokeo ya kituo zikabidhiwe kwa watendaji wanaoingiza matokeo ya kura katika Mfumo wa Matokeo ya uchaguzi (*Results Management System*) ili waendelee kufanya hivyo.

# SURA YA KUMI

## KUJUMLISHA KURA

Kwa mujibu wa kanuni ya 64 ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2020 na kanuni ya 57 ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020, Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi baada ya kupokea matokeo ya uchaguzi ya vituo vyote vya kupigia kura anapaswa kuwajulisha wagombea au vyama vya siasa vinavyoshiriki uchaguzi siku, mahali na saa ya kujumlisha kura.

### 10.1. Wanaoruhusiwa Kuwepo Wakati wa Kujumlisha Kura

Wanaoruhusiwa kuwepo wakati wa kujumlisha kura ni:-

(i) Msimamizi wa Uchaguzi;

(ii) Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;

(iii) Mratibu wa Uchaguzi wa Mkoa;

(iv) Mjumbe wa Tume;

(v) Mkurugenzi wa Uchaguzi;

(vi) Afisa wa Tume;

(vii) Mgombea;

(viii) Wakala wa kujumlisha kura;

(ix) Askari polisi au mtu anayehusika na usalama wa mahali pa kujumlishia Kura; na

(x) Mtazamaji aliyeidhinishwa na mwenye kitambulisho maalum kilichotolewa na Tume.

> **Angalizo**: Watazamaji wa Uchaguzi watapewa vitambulisho maalum kutoka Tume ambavyo vitatumika kuwatambulisha vituoni.
>
> Msimamizi wa Uchaguzi ahakikishe kuwa mtu yeyote asiyehusika asiwepo katika eneo la kujumlishia kura.

### 10.2. Maandalizi katika Sehemu ya Kujumlisha Kura

Msimamizi wa Uchaguzi ana jukumu la kufanya maandalizi ya kufanikisha zoezi la kujumlisha kura. Maandalizi hayo ni pamoja na:-

(i) Kuandaa kumbi za kujumlishia kura za Rais na Wabunge katika halmashauri na kura za Madiwani katika kata. Aidha, atakapoandaa kumbi hizo aandae: -

(a) Mahali pa kujumlishia kura;

(b) Mahali ambapo watendaji mbalimbali watafanya shughuli zao. Ikiwa ni pamoja na wale wa mfumo wa matokeo ya uchaguzi (*Results Management System);*

(c) Mahali ambapo mawakala na watazamaji wa uchaguzi watakaa; na

(d) Utaratibu wa kupokea masanduku na fomu za matokeo ya uchaguzi kutoka vituoni na mpangilio wa masanduku hayo kwenye chumba cha kujumlishia na kuandaa wasaidizi watakaomsaidia kazi hiyo,

(ii) Kuwafahamisha wagombea haki yao ya kuteua mawakala wa kujumlisha kura (wakala mmoja kwa kila mgombea);

(iii) Kuwaandaa Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi wa kutosha kwa ajili ya kujumlisha kura;

(iv) Kuandaa viburudisho;

(v) Kuandaa watendaji watakaotekeleza majukumu mbalimbali;

(vi) Kuhakikisha uwepo wa askari ili kuimarisha usalama mahali pa kujumlishia kura; na

(vii) Kuhakikisha fomu na vifaa muhimu vitakavyotumika katika kujumlisha kura vinakuwepo. Fomu na vifaa hivyo vimeoneshwa katika Jedwali Na. 3: -

**Jedwali Na. 3: Orodha ya Fomu na vifaa wakati wa kujumlisha matokeo ya uchaguzi**

| Na. | Aina ya fomu au kifaa | Matumizi fomu au kifaa |
|---|---|---|
| 1. | Fomu Na. 21A<br>SEHEMU A na SEHEMU B | Matokeo ya uchaguzi wa kiti cha Rais kituoni. |
| 2. | Fomu Na. 21B<br>SEHEMU A na SEHEMU B | Matokeo ya uchaguzi wa Ubunge kituoni. |
| 3. | Fomu Na. 21C | Matokeo ya uchaguzi wa Udiwani kituoni. |

| Na. | Aina ya fomu au kifaa | Matumizi fomu au kifaa |
|---|---|---|
| | SEHEMU A na SEHEMU B | |
| 4. | Fomu Na. 22A | Jedwali la taarifa ya jimbo kwa ajili ya matokeo ya uchaguzi wa kiti cha Rais ambayo huonesha idadi ya kura kwa kila kituo. |
| 5. | Fomu Na. 22B | Jedwali la taarifa ya jimbo kwa ajili ya matokeo ya uchaguzi wa Ubunge kwa kila kituo ambayo huonesha idadi ya kura kwa kila kituo. |
| 6. | Fomu Na. 22C | Jedwali la taarifa ya kata kwa ajili ya matokeo ya uchaguzi wa Udiwani kwa kila kituo katika kata ambayo huonesha idadi ya kura kwa kila kituo. |
| 7. | Fomu Na. 23A | Jedwali la taarifa ya matokeo ya uchaguzi wa Rais katika jimbo ambayo huonesha kura ambazo kila chama kimepata kwa kila kituo cha kupigia kura. |
| 8. | Fomu Na. 23B | Jedwali la taarifa ya matokeo ya uchaguzi wa ubunge katika jimbo ambayo huonesha kura ambazo kila chama kimepata kwa kila kituo cha kupigia kura. |
| 9. | Fomu Na. 23C | Jedwali la taarifa ya matokeo ya uchaguzi wa Madiwani katika kata ambayo huonesha kura ambazo kila chama kimepata kwa kila kituo cha kupigia kura. |
| 10. | Fomu Na. 24A | Fomu ya matokeo ya uchaguzi wa Rais, katika jimbo. Huonesha matokeo ya jimbo zima. |
| 11. | Fomu Na. 24B | Fomu ya matokeo ya uchaguzi wa Ubunge katika jimbo, huonesha matokeo ya jimbo zima. |
| 12. | Fomu Na. 24C | Fomu ya matokeo ya uchaguzi wa Udiwani katika kata, huonesha matokeo ya kata nzima. |

| Na. | Aina ya fomu au kifaa | Matumizi fomu au kifaa |
|---|---|---|
| 13. | *Projector* | Ni kifaa cha kuonesha ujumlishaji wa matokeo. |
| 14. | Vifaa vya mfumo wa usimamizi wa matokeo ya uchaguzi (*Results Management System*) kama vile *computer* | Hutumika kuingiza matokeo ya uchaguzi katika mfumo, kujumlisha na kutuma Tume. |

## 10.3. Utaratibu wa Kufuata Kabla ya Kuanza Kujumlisha Kura

(i) Kabla ya kuanza kujumlisha kura, Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atatoa maelezo kuhusu utaratibu utakaofuatwa na maadili ambayo watu waliomo katika chumba cha kujumlisha kura watapaswa kuyafuata.

(ii) Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atatoa taarifa kuhusu matukio muhimu ambayo ana habari nayo, kuhusu mwenendo wa uchaguzi kwa ujumla.

(iii) Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi awape wagombea nafasi ya kutoa maoni yao kuhusu mwenendo wa uchaguzi.

(iv) Msimamizi wa Uchaguzi atatakiwa aanze kujumlisha matokeo ya Uchaguzi wa Rais ili yaweze kutumwa Tume mapema.

## 10.4. Utaratibu wa Kufuata Wakati wa Kujumlisha Kura

(i) Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atahakikisha kwamba masanduku yote ya kura na Bahasha Na. 8A, 8B au 8C zenye Fomu Na. 21A, 21B au 21C Sehemu A na Sehemu B vimepokelewa;

(ii) Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi anaruhusiwa kufungua bahasha zifuatazo kwenye chumba cha kujumlishia kura;-

- (a) Bahasha ya Kituo,
- (b) Bahasha Na. 8A, 8B na 8C (Fomu za matokeo ya kituo)
- (c) Bahasha Na. 9 (Fomu Na. 14 na 16)
- (d) Bahasha Na. 1 (hesabu ya karatasi za kura),

(e) Bahasha Na. 3A, 3B, 3C (karatasi za kura ambazo hazikutumiwa na zilizoharibika) na

(f) Bahasha Na. 5A, 5B, 5C (kura zenye mgogoro).

### 10.5. Kutoa Uamuzi Kuhusu Kura zenye Mgogoro

Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi baada kupokea masanduku yote ya kura, taarifa zote na Fomu Na. 21A, 21B, 21C **SEHEMU A** na **SEHEMU B** atazitolea uamuzi kura zote zenye mgogoro.

Tume inashauri Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi kuwashirikisha wagombea au mawakala ili kutoa maoni yao kabla hajatoa uamuzi wa mwisho kuhusu kura zenye mgogoro. Aidha, uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi kuhusu kura yenye mgogoro utakuwa wa mwisho.

Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi baada kufanya uamuzi juu ya kura zenye mgogoro atajaza **SEHEMU B** ya fomu ya matokeo husika kwa kila uchaguzi, yaani 21A, 21B, 21C ili kuingiza kura hizo kwa kila mgombea husika, kisha wagombea au mawakala wao watatia saini katika fomu hizo. Baada ya kuzitolea uamuzi kura zote zenye mgogoro na kabla ya kujumlisha kura, Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atatangaza matokeo ya uchaguzi ya vituo vyote vya jimbo au kata kwa sauti kuanzia kituo cha kwanza hadi kituo cha mwisho.

### 10.6. Maombi ya Wakala au Mgombea ya Kurudia Kuhesabu Kura

Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atalikubali ombi la kurudia kuhesabu kura za matokeo ya uchaguzi ya kituo ikiwa usahihi wa matokeo ya uchaguzi ya kituo au vituo husika ulipingwa na wakala au mgombea katika kituo cha kuhesabia kura.

Baada ya kukamilisha zoezi hilo, Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atajumlisha kura alizopata kila mgombea.

### 10.7. Kulingana kwa Kura za Wagombea

Kwa mujibu wa kifungu cha 77 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 78 cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, pale ambapo kutakuwa na wagombea waliopata idadi ya kura inayolingana na ikashindikana kupata mshindi baada ya kujumlisha kura zote, Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi anatakiwa kufungua masanduku yote ya kura katika jimbo au kata na kuhesabu kura upya.

Baada ya kuhesabu kura zote upya na matokeo ya uchaguzi kulingana tena atatakiwa kuitaarifu Tume.

Tume itapanga siku nyingine ya uchaguzi ambayo haitakuwa zaidi ya siku thelathini (30) tangu Siku ya Uchaguzi wa awali. Wakati upigaji kura utakaporudiwa, watakaopigiwa kura ni wale tu ambao katika uchaguzi wa awali walipata kura nyingi kuliko wagombea wengine na kura zao zililingana.

### 10.8. Kujumlisha Kura za Madiwani

Kura za uchaguzi wa Madiwani zitajumlishwa katika kila kata kwa kufuata utaratibu kama ulivyoelezwa katika **sehemu ya 10.1** hadi **10. 7 ya Sura hii.**

Baada ya matokeo ya uchaguzi wa Madiwani kutangazwa katika kata, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi wa kila kata atawajulisha matokeo wagombea na/au mawakala.

**Angalizo:**

Baada ya kujumlisha kura na kutangaza matokeo ya uchaguzi, Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi wanasisitizwa kupeleka fomu na vifaa vyote kwa Msimamizi wa Uchaguzi ikiwa ni pamoja na masanduku ya kura. **Masanduku hayo hayatatakiwa kuhifadhiwa kwenye kata.**

### 10.9. Mawakala wa Kujumlisha Kura

Wagombea wanaruhusiwa kuweka mawakala katika vituo vya kujumlishia kura. Msimamizi wa Uchaguzi atatakiwa kuwafahamisha wagombea kuhusu haki yao ya kuweka mawakala katika eneo ambalo majumuisho ya kura yanafanyika.

Mawakala wa kujumlisha kura watakuwa na wajibu wa:-

(i) Kushuhudia zoezi la kujumlisha kura za Rais, Ubunge na Udiwani.

(ii) Kulinda maslahi ya mgombea kwa kuhakikisha Sheria, Kanuni na Taratibu zinazingatiwa katika zoezi la kujumlisha kura.

(iii) Kusaini fomu za matokeo ya uchaguzi; na

(iv) Kuchukua nakala ya fomu ya matokeo ya uchaguzi na kuiwasilisha kwa vyama vyao au wagombea.

**Angalizo:**

Wakala wa kujumlisha kura anapaswa kuapa kiapo cha kutunza siri mbele ya Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi siku saba (7) kabla ya siku ya uchaguzi.

# SURA YA KUMI NA MOJA

## KUTANGAZA MATOKEO YA UCHAGUZI

Baada ya kuthibitisha matokeo ya uchaguzi ya jimbo au kata husika, Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi:-

(i) Atajaza Fomu Na. 24A, 24B na 24C akionesha idadi ya wapiga kura walioandikishwa, idadi halisi ya waliopiga kura, idadi ya kura halali na idadi ya kura zilizoharibika;

(ii) Atatoa taarifa hiyo hadharani na kumtangaza mgombea Ubunge au Udiwani aliyeshinda;

(iii) Atamtaarifu rasmi mgombea aliyeshinda kwa kumpatia Hati ya Kuchaguliwa (*Certificate of Election*);

(iv) Atabandika nakala za fomu za matokeo hayo katika ubao wa matangazo nje ya kituo cha kujumlishia kura;

(v) Atatangaza matokeo ya Uchaguzi wa Rais bila kutaja mgombea aliyeshinda;

(vi) Atawapatia nakala ya fomu ya matokeo ya uchaguzi mawakala au wagombea watakaokuwepo katika kituo cha kujumlisha kura; na

(vii) Atatuma Tume nakala ya fomu za matokeo ya uchaguzi wa Rais katika jimbo, Mbunge katika jimbo na Diwani katika kata kwa kutumia Fomu Na. 24A, 24B na 24C.

Kwa uchaguzi wa Rais matokeo yajazwe katika Fomu Na 24A na yatakapokamilika yatumwe mara moja Tume. Kwa uchaguzi wa ubunge, matokeo yajazwe katika fomu Na 24B na yabandikwe nje mahali pa kujumlisha kura za jimbo. Aidha, kwa uchaguzi wa madiwani matokeo yajazwe katika fomu Na. 24C na yabandikwe nje mahali pa kujumlisha kura za kata.

Tume itatangaza kwenye Gazeti la Serikali matokeo ya uchaguzi kuonesha kura alizopata kila mgombea.

### 11.1. Taarifa ya Msimamizi wa Uchaguzi

Kwa mujibu wa kifungu cha 81(c) cha Sheria ya Taifa Uchaguzi, Sura ya 343, Msimamizi wa Uchaguzi anatakiwa kuandaa taarifa na kuiwasilisha Tume. Pamoja na mambo mengine taarifa hiyo itahusu mambo yafuatayo: -

(i) Malalamiko yaliyotolewa na wagombea au wakala na jinsi yalivyoshughulikiwa,

(ii) Maoni ya wagombea kuhusu uchaguzi, na

(iii) Matokeo ya uchaguzi.

**11.2. Kuhifadhi Nyaraka za Uchaguzi Zilizotumika**

Kwa mujibu wa kifungu cha 82 (1) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 83 (1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, Msimamizi wa Uchaguzi anatakiwa kutunza kwa usalama nyaraka zote zinazohusika na uendeshaji wa uchaguzi. Nyaraka hizo zinatakiwa ziharibiwe baada ya kupita kipindi cha miezi sita tangu Siku ya Uchaguzi isipokuwa kama kuna kesi au malalamiko ya uchaguzi (*election petition)* mahakamani.

Tume itatoa maelekezo ya utekelezaji wa suala hili kwa Wasimamizi wa Uchaguzi.

# SURA YA KUMI NA MBILI

## MAKOSA YA UCHAGUZI

Kwa mujibu wa kifungu cha 89A cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, sura ya 343 na kifungu cha 88A cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, sura ya 292, Maafisa Uchaguzi watakaofanya kwa makusudi vitendo vitakavyosababisha matokeo ya uchaguzi kutenguliwa watashtakiwa. Iwapo watapatikana na hatia watapewa adhabu ya kifungo kisichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka miwili au faini isiyopungua **shilingi laki tano (500,000/=) na isiyozidi shilingi milioni moja (1,000,000/=) au vyote kwa pamoja**.

Kwa mujibu wa kifungu cha 89B cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu 88B cha Sheria za Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, Afisa Uchaguzi atakayeisababishia Serikali hasara atatakiwa kufidia hasara hiyo kwa mujibu wa Sheria ya *The Public Officers, (Recovery of Debts) Act, Cap. 76*.

Kwa mujibu wa kifungu cha 89C cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 88C cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, Maafisa Uchaguzi ni pamoja na:-

(i) Mratibu wa Uchaguzi wa Mkoa;

(ii) Msimamizi wa Uchaguzi;

(iii) Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;

(iv) Msimamizi wa Kituo cha Kupigia Kura; na

(v) Msimamizi Msaidizi wa Kituo cha Kupigia Kura.

Pamoja na makosa tajwa hapo juu, Msimamizi wa Uchaguzi anatakiwa aelewe makosa mengine ya uchaguzi ambayo ni pamoja na:-

(i) Afisa wa Umma kutumia wadhifa wake kumkatisha tamaa mtu anayetaka kugombea;

(ii) Makosa yanayohusiana na fomu za uteuzi, karatasi za kura na masanduku ya kura kwa mfano:-

  (a) Kuharibu karatasi za uteuzi kwa makusudi;

  (b) Kughushi fomu za uteuzi;

  (c) Kughushi Karatasi ya Kura;

  (d) Kuharibu Karatasi ya Kura kwa makusudi;

  (e) Msimamizi wa kituo cha kupigia kura kuacha kugonga muhuri wa kituo kwenye karatasi ya kura kwa uzembe;

(f) Kutoa karatasi ya kura kwa mtu asiyehusika kinyume cha sheria;

(g) Kufungua sanduku la kura kinyume cha sheria;

(h) Kutangaza kwa makosa kujitoa kwa mgombea;

(i) Kutoa kiapo cha uongo; na

(j) Kutoa au kupokea rushwa.

Mtu yeyote atakayepatikana na hatia atapewa adhabu zilizotajwa katika Sheria za nchi.

# SURA YA KUMI NA TATU

## ELIMU YA MPIGA KURA

Kwa mujibu wa kifungu cha 4C cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, Tume imepewa jukumu la kutoa elimu ya mpiga kura katika Jamhuri ya Muungano, kuratibu na kusimamia taasisi zinazotoa elimu hiyo.

Elimu ya mpiga kura inalenga kumuelimisha raia kushiriki kikamilifu katika hatua mbalimbali za uchaguzi kama vile uandikishaji wa wapiga kura, kampeni za uchaguzi na upigaji kura. Tume inafanikisha jukumu hilo kwa kupitia Wasimamizi wa Uchaguzi na Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi kwa kuwa wao ndio wawakilishi wa Tume katika maeneo hayo. Hivyo, ni vema wapiga kura wapatiwe elimu hiyo kwa wakati unaofaa.

### 13.1. Utaratibu wa Kutoa Elimu kwa Mpiga Kura

(i) Tume itatoa Elimu ya Mpiga Kura, kwa kutumia njia mbalimbali kama vile: vyombo vya habari (redio, runinga, magazeti n.k), mitandao ya kijamii, mabango (*banners, posters, billboards*) vipeperushi, vikundi vya sanaa na magari ya matangazo.

(ii) Msimamizi wa Uchaguzi atapokea kutoka Tume vifaa mbalimbali kwa ajili ya utoaji wa elimu ya mpiga kura kama vile mabango na vipeperushi.

(iii) Wasimamizi wa Uchaguzi na Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi wahakikishe kuwa vifaa vyote vilivyopokelewa vinasambazwa na kubandikwa katika maeneo mbalimbali mara tu baada ya kupokelewa. Kwa mfano, sokoni, hospitali, kwenye vituo vya mabasi, shuleni, vyuoni na sehemu zenye mikusanyiko ya watu. Pia watumie magari ya matangazo kwa ajili ya kutoa elimu hiyo.

(iv) Tume itatoa vibali kwa asasi za kiraia ambazo zinatoa Elimu ya Mpiga Kura kwa umma katika majimbo na kata. Wasimamizi wa Uchaguzi watatakiwa kuzitambua asasi hizo na kufuatilia utoaji wa Elimu ya Mpiga Kura kwa niaba ya Tume.

Iwapo Msimamizi wa Uchaguzi atagundua kuwa elimu inayotolewa inapotosha na haizingatii Sheria, awashauri ipasavyo wahusika na kutoa taarifa Tume.

(v) Baada ya kukamilika kwa uchaguzi, Msimamizi wa Uchaguzi ataandika taarifa juu ya utoaji wa elimu ya mpiga kura akionesha

namna usambazaji wa vifaa ulivyofanyika na namna gari la matangazo lilivyofanya kazi na elimu hiyo ilivyosaidia umma katika uchaguzi. Taarifa hiyo ni muhimu katika kutathmini utoaji wa elimu hiyo kwa manufaa ya chaguzi zijazo.

# SURA YA KUMI NA NNE

## HITIMISHO

Wasimamizi wa Uchaguzi na Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi mnapaswa kuzingatia Maelekezo ya Tume yaliyoainishwa katika kitabu hiki katika kipindi chote cha uchaguzi. Maelekezo haya yatawasaidia katika kufanikisha majukumu yenu makubwa na muhimu ambayo mnatekeleza kwa niaba ya Tume. Tume ina imani kubwa nanyi kuwa mtatoa mchango muhimu katika kuimarisha demokrasia nchini kupitia uchaguzi.

Aidha, Wasimamizi wa Uchaguzi na Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi mnakumbushwa kutambua umuhimu wenu na wadau wengine wa uchaguzi katika kufanikisha uchaguzi huru, haki na wenye kuaminika. Vilevile, kama inavyoelekezwa kwa kila hatua, mnawajibika kutekeleza majukumu kwa uwazi, uadilifu, ushirikishaji na uaminifu wa hali ya juu kwa kuzingatia Katiba, Sheria, Kanuni za Uchaguzi, Maadili ya Uchaguzi na Maelekezo ya Tume. Ukiukwaji wowote wa sheria za uchaguzi unaweza kusababisha Watendaji wa Uchaguzi kuwajibishwa kwa mujibu wa sheria za nchi.